

Mtumiaji

Jarida la habari zenyet kuwajengea uelewa watumiaji wa huduma za Nishati na Maji

ISSN 2738-9014

Toleo Na. 10 • Julai - Desemba, 2024



HALIUZWI

Biteko aipongeza EWURA CCC utekelezaji majukumu yake



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Dkt. Doto Biteko (katikati) katika picha ya pamoja na Katibu Mkuu Wizara ya Nishati Mha. Felchesmi Mramba (kushoto), Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Dkt. James Andilile (kulia) baada ya kikao na Mwenyekiti wa EWURA CCC Mha. David Ngula (wa pili kushoto) na Katibu Mtendaji wa EWURA CCC Bi. Stella Lupimo, Bungeni jijini Dodoma mapema mwaka huu. Picha na ONWM

Sasa tuhakiki mita za maji na umeme



Kutoka Ofisi ya Katibu Mtendaji

Kwa niaba ya Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC), napenda kuwakaribisha katika toleo letu la 10 la Jarida la Mtumiaji. Jarida hili linalotoka mara mbili kwa mwaka limesheheni habari za elimu na makala za kipekee zinazolenga kuwapa maarifa na taarifa muhimu wasomaji kuhusu huduma za nishati na maji zainazodhibitiwa na EWURA.

Katika toleo hili, utapata habari na makala zinazojadili masuala mbalimbali kama vile mbinu bora za kuokoa matumizi ya nishati na maji, haki na wajibu wa watumiaji, na pia mafanikio yaliyopatikana kupitia jitihada za EWURA CCC katika kutetea maslahi ya watumiaji.

Vilevile, kupitia sehemu ya maswali yaliyoulizwa mara kwa mara, utapata fursa ya kujifunza kupitia maswali hayo, ambayo tunaamini yatakuongezea maarifa na taarifa muhimu. Sambamba na hayo, utapata kujua sheria na kanuni mbalimbali ambazo zinatumika kusimamia huduma za nishati na maji.

Tunatumaini kuwa maudhui haya yatakuwa ya msaada na yenye thamani katika kuboresha na kuongeza uelewa wako na kushiriki katika mijadala muhimu inayohusu huduma za nishati na maji. Usikose nakala yako!

Asante kwa kuwa sehemu ya juhudu zetu za kuhakikisha kuwa sauti ya mtumiaji inasikika na kuzingatiwa. Endelea kusoma na kujifunza kupitia Jarida la Mtumiaji.



Stella Lupimo
KATIBU MTENDAJI

Biteko aipongeza EWURA CCC utekelezaji majukumu yake



Na. Lugiko I. Lugiko, Dodoma

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Doto Biteko, amepongeza juhudii na kazi zinazofanywa na Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC), na kusisitiza umuhimu wa Baraza hilo kuongeza juhudii za uelimishaji kwa watumiaji wa huduma hizo.

Pongezi hizo zimetolewa wakati wa ziara ya ujumbe wa Baraza ulipotembelea ofisi ya Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu mapema Januari 2024.

Ziara hiyo iliyoshuhudiwa pia na Katibu Mkuu Wizara ya Nishati Mha. Felchesmi Mramba na Mkurugenzi Mkuu wa EWURA Dkt. James Andilile, ililenga kujitambulisha na kultambulisha Baraza kwa Mhe. Waziri Biteko.

Akitoa pongezi hizo kwa Mwenyekiti wa EWURA CCC Mhe. Biteko alisema "Nawapongeza kwa kazi kubwa mnayofanya katika jamii ya Tanzania. Ninalewa na kutambua shughuli zenu na nimekuwa nikiona machapisho yenu mara kwa mara

Bungeni. Ni muhimu kuendelea kufanya kazi kwa bidii na uadilifu ili kufikia malengo ya kuanzishwa kwa Baraza," alisisitiza Mhe. Biteko.

Mheshimiwa Biteko alisema kuwa, Baraza linao wajibu wa kufanya kazi kwa bidii na kuisaidia EWURA katika masuala yanayoangukia kwenye dhamana ya Baraza, "Najua kuna changamoto za bajeti, lakini ni muhimu kutumia rasimali zilizopo na kuongeza pia matumizi ya vyombo vya habari kwa ajili ya kuhamasiwa umma kwani kuna nguvu katika matumizi ya vyombo vya habari," alisema Mhe. Biteko.

Awali akieleza dhima ya ziara hiyo kwa Mhe. Dkt. Biteko, Mwenyekiti wa EWURA CCC Mhandisi David Ngula, alimshukuru Mhe. Biteko kwa kukubali na kuupokea ujumbe wa EWURA CCC na kuongeza kuwa ilikuwa ni shauku ya Baraza ya kufika na kulkutana na Mhe. Waziri.

Akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa majukumu kwa niaba ya Mwenyekiti wa Baraza, Katibu Mtendaji wa EWURA CCC Bi. Stella Lupimo, pamoja na mambo mengine alizishukuru Wizara ya Nishati na

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Dkt. Doto Biteko (kushoto) akisalimiana na Katibu Mtendaji wa EWURA CCC Bi. Stella K. Lupimo alipotembelewa ofisi kwa wake na ujumbe kutoka EWURA CCC mapema Januari, 2024. Dkt. Biteko alilipongeza Baraza kwa utekelezaji mzuri wa majukumu yake. Picha na Ofisi ya NWM

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji kwa ushirikiano ambao Baraza limekuwa likipata kila wakati kupitia Wizarani na EWURA.

"Mhe. Waziri, Wizara ya Nishati na EWURA zimekuwa ni wadau muhimu kwenye utekelezaji wa majukumu yake. Ni dhahiri huwezi kuta-jaja mafanikio ya Baraza pasipo kuitaja Wizara ya Nishati na EWURA. Hivyo Baraza linawashukuru wadau hawa muhimu katika utekelezaji wa majukumu yake," alieza Bi. Lupimo.

EWURA CCC kama chombo cha kumwakilisha mtumiaji wa huduma za nishati na maji nchini, itaendelea kutekeleza majukumu yake kwa weledi na kwa kujituma na kwa muji-bu wa sheria ilioianzisha.

Pongezi



Ndugu Alban Kihulla Mkurugenzi wa Huduma za Ufundzi wa Wakala wa Vipimo (WMA) akitoa maelezo kwa Ujumbe wa Baraza, ukiongozwa na Mwenyekiti wake Mha. David Ngula (wa tatu kulia) ulipofanya ziara katika mtambo wa uhakiki wa mita za umeme, Misugusugu Mkoa wa Pwani. Picha na Noela Ntiluvakule

EWURA CCC, WMA kushirikiana kumlinda Mtumiaji

Na Noela Ntiluvakule, Pwani

Mwenyekiti wa Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) Mhandisi David Ngula ametoa wito kwa Wakala wa Vipimo (WMA) kushirikiana na EWURA CCC katika kulinda masilahi ya watumiaji wa huduma za nishati na maji.

Mhandisi Ngula ametoa wito huo wakati Wajumbe wa Baraza walipotembelea ofisi za Wakala wa Vipimo (WMA) katika kituo cha uhakiki kili-chopo Misugusugu mkoa wa Pwani na kupata fursa ya kujifunza shughuli zinazofanywa na Wakala wa Vipimo.

Pamoja na mambo mengi waliyo-

jifunza wakati wa ziara hiyo Mhandisi Ngula alitoa wito huo kwa WMA kushirikiana na Baraza katika suala zima la kuwalinda watumiaji wa huduma za nishati na maji katika masuala ya vipimo hususani mita za maji na umeme.

Mhandisi Ngula alieleza kuwa siku za hivi karibuni Baraza limekuwa likipokea malalamiko mengi kutoka kwa watumiaji wa huduma za maji na nishati juu ya kuwa na mashaka na baadhi ya mita za maji na umeme kuonesha uniti nyingi tofauti na matumizi halisi.


"Sisi Baraza na Wakala wa Vipimo tuna jukumu moja kubwa la kuwalinda watumiaji hasa wale wa huduma zinazodhibitiwa na EWURA

yaani majisafi na usafi wa mazingira, nishati ya umeme, mafuta pamoja na gesi, hivyo tunapaswa kushirikiana kwa karibu katika kuhakikisha kuwa tunatimiza jukumu letu kubwa la kumlinda mtumiaji," alisema Mhandisi Ngula.

Akizungumza wakati wa ziara hiyo Katibu Mtendaji wa Baraza Bi. Stella Lupimo alisema, "Sisi kama watezezi wa watumiaji wa huduma za nishati na maji tumekuwa tukipokea kero mbalimbali mojawapo ikiwa ni kuhusu dira za maji na umeme, na nyakati fulani wateja wamekuwa wakilalamikia dira za maji kusoma upopo ama kubambikiwa bili."

Bi. Lupimo alisema, "Baraza lili-

Inaendelea Uk. 6



BODI YA UHARIRI

Ms. Stella Lupimo

- Mwenyekiti/Mhariri Mkuu
Geofrey Sokesia - Mhariri Msanifu
Lugiko L. Lugiko - Mjumbe
Chipegwa Samwel - Mjumbe
Emmanuel Chagu Paul - Mjumbe
Anadorice Komba - Mjumbe

Wachangaij

Mwasiti Athuman

Amani Mbogo

Chipegwa Samwel

Lugiko L. Lugiko

Anadorice Komba

Nuru Zuberi

Ramadhani Kakende

Emmanuel Chagu Paul

Sakina Yusuph

Zamda Mabada

Geofrey Sokesia

Brenda Magoma

Wadi Omari

Neema Nnko

Dennis Ndau

Catherine Ochido

Noela Ntiluvakule

Magreth Temba

Latifa Mzunguwanzala

Mawasiliano

**Baraza la Ushauri la Watumiaji
wa Huduma za Nishati na Maji**

Jengo la PSSSF, Kambarage Tower
Barabara ya Jakaya CCM
S.L.P. 772, Dodoma, Tanzania
Simu: +255 026 296 0099
Simu: +255 746 482 008
Baruaapepe: info@ewuracc.go.tz
Tovuti: www.ewuracc.go.tz

EwuraCCC

Mita za maji na umeme zihakikiwe

Katika ulimwengu wa sasa, ambapo rasilimali za nishati na maji ni muhimu kwa mafisha ya kila siku, ni jambo la msingi kuhakikisha kuwa watumiaji wanapata huduma hizi kwa usahihi kulingana na matumizi yao halisi. Vipimo sahihi vya mita za maji na umeme ni kipengele muhimu kinachochangia kuhakikisha kuwa watumiaji hawapati hasara na wanapata thamani ya kweli ya matumizi yao lakini pia watoa huduma hawapotezi mapato.

Vipimo vya mita za maji na umeme vinavyoendana na hali halisi ni muhimu kwa sababu mbili kuu. Kwanza, vi-nawezesha watumiaji kulipa kwa kile wanachotumia kweli, hivyo kuepuka malipo ya ziada ambayo yanaweza kusababisha mzigo wa kifedha kwa kaya nyingi. Pili, vipimo sahihi vinachangia katika usimamizi bora wa rasilimali hizi, ikiwemo kutokupoteza mapato ya mto huduma na hivyo kusaidia katika mipango ya matumizi endelevu.

Kwa kuzingatia umuhimu huu, ush-

irikiano kati ya mamlaka za maji nchini, Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), na Wakala wa Vipimo Tanzania (WMA) ni wa lazima. Mamlaka hizi zinapaswa kushirikiana kwa karibu ili kuhakikisha kuwa mita zote za maji na umeme zinazotumika na wateja wao ziwe zimehakikiwa na Wakala wa Vipimo kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizopo.

Mita zinazofanya kazi kwa usahihi na ufanisi zitapunguza malalamiko ya watumiaji kuhusu bili kubwa za maji au uwepo wa matumizi makubwa ya umeme ambayo hayaendani na matumizi yao.

Ni wito wa EWURA CCC kwamba mamlaka za maji na TANESCO kuhakikisha kuwa mita zinazofungwa kwa wateja ziwe zimehakikiwa ufanisi wake na Wakala wa Vipimo. Hii itahakikisha kuwa watumiaji wa huduma za nishati na maji wanapata huduma bora ikiwemo kulipia bili za matumizi ya huduma kulingana na matumizi yao halisi.

Kwa kushirikiana tutaweza kufikia lengo hili!

fikia uamuzi wa kutembelea Wakala wa Vipimo ili tuweze kujua mnafanye-aje kazi zenu na mnapimaje ufanisi wa dira hizi kabla hazijamfikia mteja na suala la kusema kuwa zinapima upopo likoje, ndio hasa dhima ya sisi kuwatembelea siku hii ya leo."

Akitolea ufanuzi wa hoja ziliz-oibuliwa baada ya ziara hiyo ndugu Alban Kihulla ambaye ni Mkurugenzi wa Huduma za Ufundu wa WMA, alisema kuwa, utaratibu ni kwamba Mamlaka za Maji hutangaza tenda za ununuzi wa dira, na mzabuni anayeshinda hupeleka dira hizo WMA kwa ajili ya uhakiki.

Alisema "Dira zote huja zikiwa na seal (muhuri), na WMA baada ya uhakiki huwa tunaweka "serial namba" ambayo ni namba pekee inayotofautisha dira moja na nyingine. Kitaaalamu kama dira inaweza kusoma upopo/hewa hiyo dira inakuwa hai-jakidhi viwango vya ubora na hivyo inapoteza sifa ya kuwa dira, sababu hewa au upopo huwa hausomwi katika dira. Mteja anapotilia mashaka ufanisi wa dira yake atatuandikia na

EWURA CCC, WMA kushirikiana kumlinda Mtumiaji

kufuata taratibu zilizowekwa ili dira yake iweze kuhakikiwa."

Bw. Kihulla alieleza kuwa kwa upande wa dira za umeme, WMA imekuwa ikipata changamoto kuto-kana na mwitikio hafifu wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kutupeleka dira zake katika kituo hicho na licha ya kuwepo kwa sheria inayoita-ka TANESCO kufanya hivyo.

"Jitihada mbalimbali tumezifanya mpaka sasa baada ya vikao na majadiliano mbalimbali tunatarajia kupokea dira elfu sita toka TANESCO ambazo pia ni chache maana mtambo wetu una uwezo wa kuhakiki kuanzia dira elfu nne kwa siku. Hata hivyo tu-nashukuru kwamba ni hatua kubwa

sana hatimaye mtambo wetu utaan-za kufanya kazi," alisema Bw. Kihulla.

Aliongeza kuwa katika huduma zinazodhibitiwa na EWURA kwenye sekta ya mafuta, Wakala wa Vipimo hufanya uhakiki wa vifaa vina-vyotumika kuhifadhia, kusafirishia na kuuzia mafuta kwenye maeneo mbalimbali kama vile kwenye meli zinazoleta mafuta, maghala ya kuhi-fadhia, na kwenye pampu zinazotumi-ka kuuzia mafuta kwa wateja wa rejareja katika vituo vya mafuta.

Kwa upande wa gesi, Bw. Kihulla alieleza kuwa, WMA husimamia upimaji wa kiasi cha gesi (LPG) in-ayoingia hapa nchini kutoka nje, pia hufanya ukaguzi na uhakiki wa mitungi ya gesi ya ujazo tofauti to-fauti ili kuhakikisha kuwa watumiaji wa gesi hiyo ya kupikia majumbani wanapata kiasi sahihi kulingana na thamani ya fedha wanayolipa.

Mwisho Bw. Kihulla aliahidi kushirikiana na Baraza katika kulin-da masilahi ya watumiaji wa huduma za nishati na maji hasa katika suala zima la vipimo na utoaji elimu.



Ujumbe wa Baraza, ukifuatilia kwa makini maelezo kutoka kwa Mkurugenzi wa Huduma za Ufundu WMA ndugu Alban Kihulla ya namna dira za maji zinavyo hakikiwa. Picha na Noela Ntiluvakule



Mamia wafikiwa program za uelimishaji

Na Lugiko L. Lugiko, Dodoma

Katika kipindi cha Januari hadi Juni 2024, Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) limefanikiwa kuwafikia wananchi 189,073 kuitia programu 621 za uelimishaji na kuwfundisha kuhusu mambo mbalimbali yanayohusu huduma za nishati na maji zinazodhibitiwa na EWURA.

Kiwango hiki kimevuka malengo ya kufikia idadi ya watu 48,000 iliyopangwa ambayo ni sawa na ongezeko la 293% huku idadi ya program za ueleimishaji zikiongezeka kwa 29.4% kutoka 480 hadi 621 katika kipindi cha Januari hadi Juni 2024.

Akizungumza na Jarida hili, Katibu Mtendaji wa EWURA CCC, Bi. Stella Lupimo, alieleza kwamba elimu hii ili-lenga kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu haki na wajibu wa mtumiaji wa huduma za nishati na maji, matumizi bora na endelevu ya huduma za nishati na maji pamoja na umuhimu wa matumizi ya nishati safi ya kupikia.

"Ni muhimu kwa wananchi kuelewa haki na wajibu wao ili wawewe katumia huduma za nishati na maji kwa ufanisi," alisema Bi. Lupimo na kuongeza kuwa "Kupitia programu hizi za uelimishaji, tunawapa wananchi maarifa muhimu ambayo yatawasaidia katika maisha yao ya kila siku."

Katika kueneza elimu hii, EWURA CCC imefikia makundi mbalimbali ya

jamii ikiwa ni pamoja na wanafunzi wa shule za msingi, sekondari na vyuo pamoja na walimu wao. Makundi mengine ni pamoja na wajasiriamali, waumini makanisani na misikitini, waendesha bajaj na pikipiki, pamoja na akina mama na akina baba katika vikundi vyao.

Amesema uelimishaji huo pia ulifanyika kwa umma kwa ujumla katika mikutano ya hadhara na masokoni ili kuhakikisha kila mwananchi anapata nafasi ya kujifunza na hivyo kuboresha matumizi ya huduma za nishati na maji nchini.

"Elimu ni silaha muhimu katika kuhakikisha wananchi wanatumia huduma hizi kwa uangalifu na kwa manufaa ya wote. Tunafurahia kuona mwitikio chanya kutoka kwa wananchi ambaa tumewafikia," aliongeza Bi. Lupimo.

Aidha Katibu Mtendaji huyo alieleza kuhusu mafanikio ambayo Baraza limeyapata kuitia ziara katika kituo cha Wakala wa Vipimo (WMA) kilichoko Kibaha, ambayo ililenga kuongeza uelewa wa namna bora ya kuwaelimisha watumiaji namna mita za maji zinavyofanya kazi, jambo ambalo lina mchango mkubwa katika kuimarisha uwazi na usawa kati ya watoa huduma na watumiaji, na hivyo kuimarisha ubora wa huduma zinazotolewa.

"Tunapokea malalamiko kutoka kwa watumiaji na kuyafanya kazi kwa haraka na ufanisi kwa kushirikiana na watoa huduma. Lengo letu ni kuhakikisha kila mtumiaji anapata huduma bora," alisema Bi. Lupimo.

EWURA CCC inaendelea kujidhatiti katika kutekeleza majukumu yake kwa bidii na weledi mkubwa, ili kuhakikisha watumiaji wa huduma za nishati na maji wanapata huduma bora na endelevu.

Picha ya pamoja ya Katibu Mtendaji wa Baraza, Bi. Stella Lupimo, (aliyeketi katikati) akiwa na Maafisa Wasaidizi Huduma kwa Wateja kutoka mikoa mbalimbali yenye ofisi za Baraza, mara baada ya kuhitimisha mafunzo kwa watumishi hao yaliyotolewa na Chuo cha Mafunzo, Diplomasia na Uchumi, mjini Bagamoyo mwezi Mei 2024.
Picha na Mpigapicha Wetu

kuhusu dhana ya bili kubwa za maji zinazoweza kusababishwa na ufanyaji kazi wa mita iliyofungwa kwa mteja," alisema Bi. Lupimo.

Kuhusu upokeaji na ushughulikiaji wa malalamiko kwa kipindi tajwa, Baraza limepokea na kusaidia utatuza wa jumla ya malalamiko 2,760 kutoka kwa watumiaji wa huduma za nishati na maji. Miongoni mwa hayo, malalamiko 1,363 ni ya umeme, 24 ni ya mafuta, 18 ni ya gesi na 1,355 ni ya maji.

Katika kushughulikia malalamiko hayo, EWURA CCC ilishirikiana kwa karibu na watoa huduma kuhakikisha changamoto zinazokabili watumiaji zinatatuliwa kwa haraka na ufanisi. Ushirikiano huu umesaidia kuboresha uhusiano kati ya watoa huduma na watumiaji, na hivyo kuimarisha ubora wa huduma zinazotolewa.

"Tunapokea malalamiko kutoka kwa watumiaji na kuyafanya kazi kwa haraka na ufanisi kwa kushirikiana na watoa huduma. Lengo letu ni kuhakikisha kila mtumiaji anapata huduma bora," alisema Bi. Lupimo.

EWURA CCC inaendelea kujidhatiti katika kutekeleza majukumu yake kwa bidii na weledi mkubwa, ili kuhakikisha watumiaji wa huduma za nishati na maji wanapata huduma bora na endelevu.

Baraza lasogeza elimu kwa umma



Na Latifa Mzunguwanzala, Dar es Salaam

Baraza la Ushauri la Watumiaji Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) lilishiriki katika Maonesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa (DITF) Sabasaba mwaka 2024 yaliyofanyika kwenye viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere, Dar es Salaam.

Maonesho hayo, yaliyoanza Juni 28 na kumalizika Julai 13, 2024, yalibeba kauli mbiu ya "Tanzania Mahali Sahihi pa Biashara na Uwekezaji."

EWURA CCC kuitia maonesho hayo ilitoa elimu kwa wadau mbalimbali waliofika katika banda lake huku likiwaahidi ushirikiano na utetezi wa maslahi yao.

Lugiko Lugiko, Afisa Uhamasishaji na Uelimishaji kutoka EWURA CCC, alisitisiza kuwa Baraza limejipanga vyema kuwawakilisha watumiaji wa huduma za nishati na maji wa makundi yote, kuanzia mtu mmoja mmoja, taasisi, viwanda na hata wawekezaji kutoka nje ili kuhakikisha kuwa wanapata huduma bora kutoka kwa watoa huduma.

"Baraza limejipanga vyema kuwatumikia watanzania na wageni kutoka nje wanaokuja kuwekeza nchini ili ku-

hakikisha maslahi yao katika huduma za nishati na maji yanazingatiwa. Pia tunawasisitiza watumiaji kuzingatia wajibu wao kwa kuwa na matumizi sahihi na salama, kujiepusha na uhujumu wa miundombinu ya huduma husika kama vile kujiunganishia huduma bila kufuata taratibu na kulipa ankara zao kwa wakati, lakini pia kudai fidia wana-pokuwa wameumizwa na watoa huduma kwa namna moja au nyingine," alisema Lugiko.

Baadhi ya washiriki wa maonesho hayo walitembelea banda la EWURA CCC walionekana kuvutiwa na kazi zinazofanywa na Baraza.

Geoffrey John, mkazi wa Tabata, alisema, "Kiukweli nimefurahi na nawashukuru sana EWURA CCC kwa elimu hii mliyonipa kuhusu huduma za maji, mafuta, gesi na umeme. Nimeeongeza uelewa wa kutumia huduma hizi kwa makini na kuwa nitajitahidi kuzingatia matumizi sahihi ili kuepuka hatari kama vile za moto."

Mwajuma Shabani, mkazi wa Mbezi, alisema, "Leo nimejua tofauti ya EWURA CCC na EWURA. Nilijua nyie ndio EWURA, lakini sasa nimeelewa nyie ni Baraza, ambacho ni chombo cha kutuwakilisha sisi watumiaji wa huduma za nishati na maji. Nashukuru

Mwenyekiti wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Mkoo wa kikazi Temeke, Bi. Neema Swagara (kulia) akitoa elimu kwa watumiaji waliofika katika banda la EWURA CCC kwenye Maonesho ya 48 ya Kimataifa ya Biashara Sabasaba, katika Viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam.

Picha na Latifa Mzunguwanzala

sana kwa elimu hii mliyotupatia."

Maonesho hayo yalifunguliwa rasmi siku ya Jumatano tarehe 3 Julai, 2024 na Rais wa Msumbiji, Mh. Filipe Jacinto Nyusi, aliyealikwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mh. Dkt Samia Suluhu Hassan kwa ziara ya siku nne hapa nchini na kufung-wa rasmi siku ya Jumamosi tarehe 13 Julai, 2024 na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi.

Aidha, EWURA CCC inaendelea kutoa elimu kwa wananchi kuitia Kamati za watumiaji wa huduma za nishati na maji zilizoko katika mikoa yote ya Tanzania bara, ili kuhakikisha wananchi wanapata uelewa sahihi juu ya haki zao, wajibu wao na jinsi ya kushughulikia malalamiko yao na kutumia huduma hizo kwa usahihi.

Nani mwenye idhini ya kuwasilisha malalamiko EWURA?

Na Noela Ntiluvakule, Pwani

Watumiaji wa huduma za nishati na maji wamekuwa wakipata hasara na changamoto mbalimbali kutokana na matumizi ya huduma za umeme, maji, mafuta, na hata gesi.

Hata hivyo, pamoja na kupata changamoto hizo, watumiaji wengi wamekuwa hawajui ni kwa namna gani wanaweza kuwasilisha malalamiko kwenye mamlaka husika na wakasaidiwa kupata haki zao.

Wananchi wengi hawajui ni nani mwenye mamlaka ya kuwasilisha lalamiko EWURA pale inapotokea hasara au changamoto yeyote itokanayo na huduma za nishati na maji, hii ndio sababu ya wengi wao hukaa kimya na haki zao kupotdea.

Kwa mfano ikiwa unaishi kwenye nyumba ya kupanga na ikatokea hitilifu ya umeme na ukaunguliwa na vifaa vyako vya umeme, je unafahamu kuwa wewe mpangaji unaweza ukawasilisha lalamiko lako EWURA?

Kwa mujibu wa kifungu namba

34(2) (a) cha Sheria ya EWURA, Sura Na. 414 ya mwaka 2006 inaelekezwa kuwa mlalamikaji sahihi ni yule am-baye ana maslahi katika suala linalohusiana na lalamiko lake. Kanuni za EWURA za kutatua migogoro GN. No. 428, mwaka 2020 zinabainisha kwa kutaja watu ambao wanaweza kuwa walalamikaji sahihi kama ifuatavyo:

1. Mtumiaji yeyote anaweza kuwasilisha malalamiko dhidi ya msambazaji wa huduma inayodhibitiwa na EWURA kuhusiana na jambo lolote linalohusiana na huduma za nishati na maji. Kwa mfano, mteja anaweza kulalamika kwa kudai fidia baada ya kuunguliwa na nyumba au vifaa vyake vinavyotumia umeme baada ya kuwa amewasiliana na mtoa huduma na ikikosekana suluhu mlalamikaji huyo anaweza kujaza fomu ya malalamiko ya EWURA kwa ajili ya kupata utatuzi zaidi.

2. EWURA CCC inaweza kuwasilisha lalamiko au malalamiko ya jumla yanayoathiri maslahi ya umma katika sekta husika inayodhibitiwa na EWURA. Kwa mfano inapotokea mtuu au eneo fulani wanapata changamoto ya huduma za nishati na maji na kusiwe

na mtu yeyote toka eneo husika aliye lalamikia changamoto hiyo, EWURA CCC inaweza kulalamika kwa niaba ya watumiaji wa eneo husika.

3. Mwakilishi aliyeidhinishwa anaweza kwa niaba ya mtumiaji yeyote kuwasilisha malalamiko kwa EWURA. Mfano mpangaji anaweza kulalamika kwa niaba ya mwenye nyumba endapo mwenye nyumba atakuwa amemuidhinisha kwa maandishi au kisheria kufanya hivyo pindi mwenye nyumba anapokuwa hayupo katika eneo linaloathirika. Pia mwakilishi anaweza kulalamika kwa niaba ya watumiaji wenye mahitaji maalumu na wasiojiweza.

4. Pia kundi la watu walioathirika au wanaoathirika wanaweza kuwasilisha lalamiko lao EWURA kama kanuni ya (4), (a) na (b) ya Kanuni tajwa hapo juu inavyoeleza. Waathirika hao wanaruhusiwa kuwasilisha lalamiko lao kwa kujaza fomu ya malalamiko na kuambatanisha orodha ya majina ya wahusika na saini zao au alama za vidole gumba wakiambatisha muhtasarri wa mkutano uliofanyika na kuruhusu uwasilishaji wa lalamiko.

Mtu mwininge nje ya hao waliota-jwa hawesi kuwa na idhini ya kulalamika juu ya huduma zinazodhibitiwa na EWURA. Mlalamikaji anapokuwa sio sahihi inaweza kuwa ni moja ya sababu inayopelekea lalamiko kukata-liwa.

Malalamiko



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAJI
MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA
MAKONDE (MPWSSA)**



**KULIPA BILI YAKO MAPEMA
NI UZALEENDO**















Mitandoa ya Kijamii:
Mamlaka ya Maji Makonde



Piga Namba Hii Bure:
0800 71 0920

uk. 9

Mtumiaji • Toleo Na. 10 • Julai - Desemba, 2024

Elimu ya mtumiaji sasa hadi msikitini

Na Mwandishi wetu, Dodoma

Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) mkoani Dodoma limekujaa na mpango wa kuwafikia watumiaji katika Misikiti ya Dodoma mjini ili kuwajengea uwezo wa wafahamu masula yanayohusu huduma za nishati na maji, kuzijua haki zao na kufahamu wajibu wao kama watumiaji wa huduma hizo zinazodhibitiwa na EWURA.

Mpango huo wa uelimishaji ni matokeo ya mazungumzo kati ya ofisi ya EWURA CCC na Sheikh Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Sheikh Mustapha Rajabu Shabani, yaliyofanyika mnamo tarehe 10/6/2024 kuomba kufanya shughuli za uelimishaji katika misikiti iliyopo jijini Dodoma ambayo ipo chini yauongozи wake.

Sheikh Mkuu wa Mkoa alipokea vyema ombi hilo la EWURA CCC na kukubaliana na mpango huo wa utoaji elimu Misikitini akisema kuwa, elimu hiyo ni muhimu kwa waumini wake kwani itasadia

kuongeza uelewa kuhusu huduma za nishati na maji ikiwemo matumizi sahihi, salama na endelevu ya huduma za nishati na maji.

"EWURA CCC mnafanya kazi nzuri na ninakubaliana na mpango wenu wa kuelimisha waumini wetu katika Misikiti juu ya huduma za nishati na maji. Elimu kutoka kwenu itakuwa msaada kwa waumini na familia zao lakini hata kwa uendeshaji wa shughuli za ibada," alisema Sheikh Mustapha.

Aliongeza kuwa wakati mwingine waumini hutumia vibaya rasilimali hizi zikiwemo maji kwa kuacha yanamwagika ovyo na hivyo kuongeza ghamama za uendeshaji katika nyumba hizo za ibada. Tunaamini elimu hiyo itasaidia waumini wetu kuongeza umakini wa kutumia vyema na kutunza rasilimali hizi.

Naye Afisa Tawala BAKWATA Mkoaa, ndugu Yusuph Marengu aliunga mkono suala la EWURA CCC kutoa elimu katika misikiti baada ya Sheikh Mkuu wa Mkoa kukubaliana na mpango huu.

"Ninaungana na Sheikh wetu

wa Mkoa kuwa elimu hii itolewe katika misikiti yetu kwani huduma za nishati na maji zinagusa watu wa makundi yote katika jamii yetu, hivyo kuwa na uelewa sahihi wa matumizi yake zikiwemo sheria na kanuni ni jambo la muhimu sana," alisema Bw. Yusuph.

Naye Sheikh wa Msikiti wa Masjid Riyadhawa-Kikuyu, Sheikh Shafi Ramadhan alisema kuwa Baraza linakaribishwa kwa ajili ya kutoa elimu kwa waumini kama ambavyo Sheikh Mkuu wa Mkoa ameagiza ifanyike katika misikiti ya Dodoma mjini.

"Nikiwa Sheikh wa Msikiti huu, ninawakaribisha sana kutoa elimu hii katika Msikiti wetu na nitawapa ushirikiano wa kutosha. Ni matumaini yangu kuwa elimu hii itasambaa kwa watu wengine ambao hawapo hapa Msikitini," alisema Sheikh Shafi.

EWURA CCC mkoani Dodoma imeanza utekelezaji wa mpango huu kwa kuanza kutoa elimu katika Msikiti wa Riyadhawa-Kikuyu ambaapo zaidi ya watu 100 wamefikiwa.



Afisa Msaidizi Huduma kwa Wateja na Utawala Bw. Amani Mbogo akitoa elimu kwa waumini wa Msikiti wa Riyadhawa-Kikuyu kuhusu matumizi sahihi ya huduma za nishati na maji. Picha na Bilson Vedastus

RCC Kilimanjaro yajipanga kutekeleza majukumu yake

Na Zamda Mabada, Kilimanjaro

Wajumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma zinazodhibitiwa na EWURA mkoa wa Kilimanjaro (RCC) wameahidi kushirikiana katika kufanya kazi ili kufikia malengo ya Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) katika ngazi ya mkoa.

Akiongea hayo wakati wa kikao cha utambulisho na kupanga mikakati ya utekelezaji wa majukumu ya Baraza kilicho fanyika mapema mwaka huu katika ofisi za EWURA CCC mkoa wa Kilimanjaro, Mwenyekiti wa Kamati Bw. Josephat Mmbonyo alianza kwa kuwaponeza Wajumbe wa Kamati hiyo kwa kuteuliwa na Baraza na kuonesha utayari wa kuwatumilia watumiaji wa huduma za nishati na maji ndani ya mkoa wa Kilimanjaro.

Mwenyekiti huyo aliaahidi Wajumbe wa Kamati hiyo kuwa yeye yupo tayari kutoa mchango wake na

ushirikiano kwa Kamati katika kutekeleza majumu yao na ili kufikia malengo ya Kamati na Baraza kwa ujumla.

"Nawapongeza Wajumbe wenzangu kwa kuteuliwa kwenu, ninaamini kuwa baada ya mafunzo ya kutujengea uwezo tuliyopata tutaenda kuyafanya kazi katika mkoa wetu ili kuleta tija zaidi," aliezeza Bw. Mmbonyo

Bw. Mmbonyo aliongeza kuwa anaamini Wajumbe hao wakishirikiana kwa ukaribu basi Kamati yao itakuwa na uwezo wa kufanya makubwa katika kulitangaza Baraza na kusaidia kutatua changamoto ambazo zinawakabili watumiaji wa huduma za nishati na maji ndani ya mkoa wa Kilimanjaro.

"Naomba mnipe ushirikiano nami nitawapa ushirikiano wa kutosha ili tutekeleza jukumu letu la msingi la kulitangaza Baraza na kuwatetea na kulinda masilahi ya watumiuaji wahuduma hizi zinazo dhibitiwa na EWURA," alisema Mmbonyo

Naye Mjumbe wa Kamati hiyo Bi. Debora Mwamponda alilishukuru Baraza kwa kuwaamini na kuwateua kuwa wajumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji mkoani humo lakini pia kuwajengea uwezo katika kutekeleza majukumu yao kama wanakamatii.

"Nalishukuru Baraza kwa kututeua kuwakilisha watumiaji katika mkoa wetu, nasi tunaahidi kwenda kutumia elimu tuliyopata kwenye mafunzo hivi karibuni katika kutetea watumiaji wa maji na nishati katika mkoa wetu," alisema Bi. Mwamponda.

Aliwasilitiza wajumbe wenzake kuwa ili waweze kutekeleza vyema majukumu yao ni lazima wajumbe washirikiane na kutumia nafasi zao katika jamii katika kutoa elimu kwa wananchi kuhusu masuala yanayohusu bidhaa na huduma za nishati na maji ili wananchi waweze kutambua haki na wajibu wao kama watumiaji.

Aidha kwa upande wake Mjumbe mzoefu aliyeteuliwa kwa awamu nyininge Bw. William Luanda aliwapongeza na kuwakaribisha Wajumbe wenzake kwa kuwaahidi kutoa ushirikiano na uzoefu wake kwenye Kamati ili kuhakikisha watumiaji wanafurahia huduma za nishati na maji ndani ya mkoa huo.

"Sisi wajumbe ni watekelezaji wakubwa wa mipango na mikakati ya Baraza. Kwa umuhimu huo tunapaswa kushirikiana ili kutekeleza lengo la kuwatetea watumiaji. Nasilitiza umuhimu kushirikiana kati yetu kwenye kupanga na kutekeleza majukumu ya Kamati pia kuwe na mahusiano mazuri kati yetu kufikia malengo. Kwa kufanya hivi itatuweka katika nafasi nzuri kutimiza malengo makubwa ya kuwepo kwa Kamati yetu," alisema Bw. Luanda.

Kifungu cha 31(1) (c) cha Sheria ya EWURA Sura namba 414 kinaeleza kuwa katika kutekeleza majukumu yake, Baraza litaunda Kamati za watumiaji katika mikoa mbalimbali nchini na kushauriana nazo. Mapema mwaka huu Baraza lilizindua Kamati zake za mikoa zilizopo katika mikoa yote 30 Tanzania bara anbazoo zinawandwa na Wajumbe watano kwa kila mkoa, lengo likiwa ni kusogezza huduma zake kwa watumiaji wa huduma za nishati na maji katika ngazi za mikoa.

Makala



Baraza laponcezwa uelimishaji ngazi ya mitaa

Na Dennis Ndanu, Mara

Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) mkoani Mara limeponcezwa kwa kazi zake za kutoa elimu ya matumizi sahihi ya huduma, haki na wajibu wa mtumiaji na namna ya kuwasilisha na kutatta malalamiko ya watumiaji.

Pongezi hizo zimetolewa mkoani Mara na Mwenyekiti wa Serikali ya mtaa wa Makoko Ziwani ndugu Paschal Rukomba Mato, kufuatia shughuli za uelimishaji zilizokuwa zikifanywa na Kamati ya Watumiaji wa Huduma zinazodhibitiwa na EWURA kupitia mikutano ya hadhara katika ngazi ya mtaa.

Mato ambaye alialika Kamati ya

Watumiaji ya Baraza mkoani Mara kutoa elimu kupitia mikutano wa hadhara katika mtaa wa Makoko Ziwani alisema kuwa, elimu kuhusu haki na wajibu wa watumiaji imefungua macho wananchi waliohudhuria mikutano huo.

"Nawapongeza sana EWURA CCC mkoani Mara kwa kuona umuhimu wa kuwafuata wananchi katika ngazi ya mitaa na kuwapatia elimu ya matumizi ya huduma za nishati na maji. Wengi wetu hatukuwa tunajua hata taratibu za kufikisha malalamiko yetu kwa watoa huduma, mimi ni-kiwa mmoja wao lakini kwa sasa nimejua haki zangu na wajibu wang'u kupitia elimu miliyotoa," alisema Bw. Mato.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Kamati ya Watumiaji mkoani

Mara ndugu Robinson Wangaso aliushukuru uongozi wa Serikali ya Mttaa kwa kulipatia Baraza fursa ya kutoa elimu kwa wakazi wa eneo hilo.

"Tunaushukuru uongozi wa Mttaa kwa fursa hii adhimu tuliyopata kuelimisha wananchi. Tunaomba ushirikiano huu uendelee ili hata kwa nyakati zijazo Baraza liweze kuwafikia watu wengi zaidi na kuwapatia elimu na taarifa muhimu katika matumizi ya huduma za nishati na maji," alisema Bw. Wangaso.

Wangaso aliongeza kuwa Baraza na Kamati yake mkoani Mara iko tayariki kuwafuata wananchi mahali waliko ili kuwapatia elimu stahiki kwa matumizi bora na endelevu kuhusu huduma za nishati na maji zinazodhibitiwa na EWURA.



MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MBEYA (MBEYA WSSA)



BEI ZA MAJI NA HUDUMA ZINGINE

Bei za maji za sasa na zilizoidhinishwa (Shilingi kwa Mita ya Ujazo)

Kundi la Wateja	Matumizi (m ²)	Bei Zilizoidhinishwa			
		2023/24	2024/25	Sh./m ²	Sh./20L
Majumbani	0-10				
	10-20	1,400	28	1,560	31.2
	>20				
Taasisi	0-30				
	>30	2,000	40	2,130	46.2
Bishara	0-30				
	>30	1,820	36.4	2,130	46.2
Vivanda	0-50				
	>50	2,100	42	2,400	48
Magati		1,250	25	1,500	30
Bora		2,700	54	2,700	54

Ada za sasa na Zilizoidhinishwa kwa Maunganisho Mapya ya Maji

Kundi la Wateja	Ada Iliyoidhinishwa	
	2023/24	2024/25
Majumbani	26,000	26,000
Taasisi	26,000	26,000
Bishara	26,000	26,000
Vivanda	26,000	26,000

Huduma kwa wateja piga 0800110088 bure

Tozo za sasa na zilizoidhinishwa za Kurejeshewa Huduma ya Maji

Kundi la Wateja	Tozo Zilizoidhinishwa	
	2023/24	2024/25
Majumbani	20,000	20,000
Taasisi	30,000	30,000
Bishara	35,000	35,000
Vivanda	45,000	50,000

Tozo za Sasa na Zilizoidhinishwa za Huduma ya Majitaka (Shilingi kwa Mita za Ujazo)

Kundi la Wateja	Tozo Zilizoidhinishwa	
	2023/24	2024/25
Majumbani	450	500
Taasisi	590	650
Bishara	670	740
Vivanda	830	920

Tozo za Sasa na Zilizoidhinishwa za Huduma ya Majitaka kwa wateja wasio na Huduma ya Maji (Shilingi kwa Mwezi)

Kundi la Wateja	Tozo Zilizoidhinishwa	
	2023/24	2024/25
Majumbani	22,500	23,000
Taasisi	28,300	31,400
Bishara	42,400	47,000
Vivanda	42,400	45,000

Tozo za Sasa na Zilizoidhinishwa za Kumwaga Majitaka kwenye Mabwawa ya Mbeya UWSSA (Shilingi kwa tripu)

Kundi la Wateja	Tozo Zilizoidhinishwa	
	2023/24	2024/25
Magari yote	17,500	17,000

MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA (MBEYA WSSA)

S.L.P 2932 MBEYA Simu: +2550252504298 Fax: +2550252503492

Email: md@mbeyawssa.go.tz

Watengenezaji majiko ya mkaa wafundwa

Na Mwasiti Athuman, Mbeya

Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Mkao wa Mbeya imetoa elimu kwa watengeneza majiko ya mkaa na wanunuzi wa vyuma chakavu kwa kushirikiana na wadau wa nishati safi ya kupikia kuto Taifa Gesi.

Uelimishaji kwenye makundi hayo ya watumiaji umetokana na wimbi la kuibwa na kupotea kwa mitungi ya gesi (LPG) katika baadhi ya mitaa jijini Mbeya ambapo impelekeza Baraza kwa kushirikiana na Kampuni ya Taifa gesi kutoa elimu juu ya madhara ya kununua mitungi ya gesi kama malighafi ya kuzalisha bidhaa ikiwa imekatwa katwa kama

chuma chakavu katika mtaa wa Il-embo, kata ya Iyela jijini Mbeya.

Happy Myahudi, mkazi wa Mtaa wa Ilembo anasema aliabiwa mitungi wa gesi na kuukuta baada ya wiki moja ukiwa umeharibiwa na kulazimika kununua mitungi mwingine wa gesi, jambo liliomwingizia gharama ambazo hakuwa amepanga.

Mjumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji mkoani Mbeya ndugu Lusekelo Kajela, amewataka wafanyabiashara wa chuma chakavu na watengeneza majiko ya mkaa kuwa waaminifu na kuepuka kujihusisha kununua malighafi ambazo zinaweza kuwa zitemtokana na wizi.

"Niwasihii tuijepushe kununua mitungi ya gesi na kuitumia kwa ma-

tumizi ya chuma chakavu, ni hatari kwa usalama na pia jambo hili husababisha hasara kwa makampuni ya gesi ambayo yanachagiza matumizi ya nishati safi nchini," alisema Bw. Kajela.

Joseho Mwashinga ampaye ni mtengeneza majiko na mnunuzi wa vyuma chakavu anasema, alikuwa hafahamu kuwa kununua mitungi ya gesi iliyokatakatwa kuwa ni kinyume cha sheria na kuishukuru EWURA CCC kwa kushirikiana na Taifa Gesi kwa kuwapa elimu hiyo nzuri.

"Nilikuwa sijui kuwa kununua mitungi ya gesi iliyokatwa ni kinyume cha sheria. Nashuku EWURA CCC na Taifa Gesi kwa elimu hii muhimu," alisema ndugu Mwashinga.

Ushauri

HabariPicha



Katibu Mtendaji wa Baraza, Bi. Stella Lupimo, akiuliza swali kwa Mha. Fabian Maganga, Mkurugenzi wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira (IRUWASA) wakati wa ziara ya Wajumbe wa Baraza, IRUWASA hivi karibuni. Hapa ni Kitwiru, moja ya maeneo yaliyotembelea ambako kuna chanzo cha maji cha chemchemi kinachotumiwa na IRUWASA. Ziara hiyo ilifanyika mapema Mei, 2024. Picha na Brenda Magoma



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mhe. Albert Chalamila (kushoto) akipokelewa na Katibu Mtendaji wa EWURA CCC (kulia) Bi. Stella Lupimo wakati wa kilele cha Maadhimishi ya Siku ya Mtumiaji duniani. Maadhimisho haya yaliyafanyika katika Ukumbi wa Karimjee, jijini Dar es Salaam, tarehe 15 Machi, 2024 Picha na Mpigapicha Wetu




Wajumbe wa Baraza wakiongozwa na Mha. David Ngula (wa pili kulia) katika picha ya pamoja na Mha. Nyirabu Musira (katika) wakati wa mafunzo ya kuwajengea uwezo Wajumbe wa Kamati za Mikoa za Baraza, mjini Morogoro. Picha na Mpigapicha Wetu

HabariPicha



Mkurugenzi Mkuu EWURA, Dkt. James Andilile (kushoto) akieleza jambo alipotembelea banda la EWURA CCC wakati wa Maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma, yaliyofanyika mwezi Juni 2024, jijini Dodoma. Wengine ni Katibu Mtendaji wa Baraza Bi. Stella Lupimo (katikati), Meneja Rasilimali Watu na Utawala, EWURA Bw. George Seni (wa pili kushoto), Kaimu Afisa Uelimishaji na Uhamasishaji, Lugiko L. Lugiko (wa pili kulia), na Afisa Msaidizi Huduma kwa Wateja, Bw. Amani Mbogo (wa kwanza kulia), wote kutoka EWURA CCC. Picha na Mpigapicha Wetu



Mwenyekiti wa Baraza Mha. David Ngula akitoa hotuba ya ufunguzi wakati wa mafunzo ya kuwajenega uwezo Wajumbe wa Kamati za Mikoa za Baraza yaliyofanyika mwezi Februari, 2024 mjini Morogoro. Picha na Mpigapicha Wetu



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Bi. Rosemary Senyamule (kushoto) akipokea Jarida la Mtumiaji alipotembelea banda la EWURA CCC wakati wa kilele cha Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma, 2024 jijini Dodoma. Picha zote na Mpigapicha Wetu


Ukweli kuhusu ukaguzi wa mifumo ya umeme katika majengo

Na Anadorice Komba, Kagera

Uzoefu unaonesha watu wengi baada ya kupata huduma ya umeme katika nyumba zao huwa hawafanyi ukaguzi wa miundombinu ya umeme na hali hii hupelekea majanga mbalimbali kama vile umeme

kupotea, ajali ya kuunguliwa na vifaa vya umeme na hata nyumba kulipuka au kupoteza maisha ya watu.

Sheria ya Umeme ya Mwaka 2008, inaeleza kuwa miundombinu ya mto huduma wa umeme (TANESCO) inaishia kwenye mita inayopima kiwango cha matumizi ya mteja, na eneo hilo ndilo mto huduma hu-



Moja ya picha inayoonyesha namna mfumo wa umeme unavyosukwa katika majengo.
Picha kwa hisani ya tovuti:<https://images.app.goo.gl>

wajibika nalo.

Wakati huo, eneo la kutokea kwenye mita kuingia ndani ni wajibu wa mteja kuhakikisha miundombinu yake ni salama kupata huduma ya umeme, na hivyo kwa mtumiaji wa umeme, kufanya ukaguzi wa mifumo na miundombinu yake ni jambo la muhimu sana kwa usalama wake.

Kanuni za Umeme, Ufungaji wa Mifumo ya Umeme za 2022 Tangazo la Serikali Namba 113, Jedwali la 3 zinaonesha kuwa kwa nyumba ya makazi, ukaguzi unapaswa ufanyike kila baada ya miaka mitano, kwa viwanda ukaguzi ufanyike ndani ya miaka mitatu, nyumba za biashata ni kila baada ya miaka minne, nyumba za umma ni kila baaada ya miaka mitatu na majengo mengine yote ni kila baada ya miaka miwili.

Ziko faida kadha za kufanya ukaguzi huo, na miongini mwake zinaleezwa katika Makala hii:

■ Usalama

Ukichunguza mfumo wa umeme katika nyumba yako inakuahakikisha usalama wa familia yako na mali zako. Nyaya zilizokaa muda mrefu zina tabia ya kuoza au kuchubuka, na hivyo ikitokea zikagusana zinaweza kuleta hatari kubwa hasa kwa wato-to, kwa sababu hawawezi kujua hatari iliyopo.

Jambo la kuzingatia wakati wa kuchunguza mifumo ya umeme ni kutumia mafundi wenye leseni ya EWURA. Kwa mujibu wa kifungu cha 19 (1) cha Sheria ya Umeme, Sura ya 131 ya mwaka 2022 inam-taka mwenye jengo kumwajiri fundi mwenye leseni ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA).

■ Huepusha kuzidisha matumizi katika mfumo wa umeme

Unapochunguza miundombinu ya umeme na fundi kugundua tatizo atakupa ushauri nini cha kufanya iki-wemo kuona uhitaji wa kuongeza au kupunguza vifaa vya umeme ili vifanye kazi kwa ufanisi.

■ Kudhibiti umeme kuvuja

Unapofanya ukaguzi wa mifumo ya umeme katika nyumba yako, inasaidia kuokoa pesa kwenye manunuzi ya umeme kila mara kwani ukaguzi utakuwezesha kubaini endapo kuna mahali umeme unavuja.

Ni mihumu kuzingatia muda wa ukaguzi uliowekwa ili kujiepusha na athari zinazoweza kujitokeza.

Fahamu utaratibu wa kuomba leseni ya rejareja ya biashata ya mafuta

Na Amani Mbogo, Dodoma

Kanuni za Uendeshaji wa Biashara ya Mafuta ya Rejareja za Mwaka 2022 GN. 150(12(a-e) zinamtaka mfanyabiashara wa mafuta aina ya petroli wa rejareja aombe na kupewa leseni kutoka EWURA. Kwa mujibu wa kanuni hizi, leseni hiyo ndio ruhusa inayotolewa kufanya shughuli inayodhibitiwa na EWURA katika bishara hiyo.

Makala hii inaangazia utaratibu wa kuomba leseni ya kuuza mafuta rejareja.

Mwombaji ye yote wa leseni ya rejareja ya mafuta, sharti afanye maombi kwa njia ya kieletroniki kupitia tovuti ya EWURA. Taarifa zinazohitajika kuambatanishwa katika maombi hayo ni kama ifuatavyo:

- Nakala ya nyaraka za usajili wa kampuni au leseni ya biashara.

- Nakala ya hatimiliki ya kiwanja palipojengwa kituo cha mafuta au uthibitisho kutoka mamlaka husika iliyoruhusu ujenzi wa kituo.
- Nakala ya kibali cha ujenzi kutoka Halmashauri au Manispaa husika
- Nakala ya cheti cha tathmini ya athari ya mazingira (Environmental Impact Assessment Certificate) kinachotolewa na Baraza la Hifadhi ya Mazingira.
- Nakala ya cheti cha mlipa kodi (TIN Certificate)
- Nakala ya cheti cha zimamoto (Fire Safety Certificate) kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani
- Kibali cha ujenzi kutoka EWURA (kwa vituo viliyoyojengwa baada ya April 2009)
- Orodha ya miundombinu ili yopo katika eneo hilo. Kwa upande wa matanki uoneshwe ujazo wake.
- Mchoro wa kituo ambao ume-sainiwa na mhandisi aliyesajiliwa

na Baraza la Wahandisi Tanzania ukionesha yafuatayo:

- Umbali uliopo kati ya Miundombinu ya kituo cha mafuta,
- mahali pa kuingia na kutokea kituoni,
- Mpaka wa Kiwanja, na
- Mahali pampu zinapotegemewa kufungwa.

- Stakabadhi ya malipo ya ada ya maombi ya kibali cha ujenzi ambayo ni shilingi laki tano
- Kumbuka kuwa Nyaraka 1-6 sharti zihakikiwe na Kamish-na wa viapo.

Kituo cha mafuta kinachokidhi masharti tajwa, ndicho hupewa leseni na EWURA. Vituo vya mafuta ambavyo havikidhi masharti ya kupewa leseni, haviruhusiwi kufanya biashara hadi hapo vitakapokuwa vimekidhi masharti yote. EWURA CCC inawahimiza watumiaji wa huduma za mafuta zinazodhibitiwa na EWURA kununua mafuta katika vituo vyenye leseni na viliyoidhishwa na EWURA kwa ajili usalama na uhakika wa huduma hizo.

Uelimishaji



JE, UMELIPA BILI YAKO YA MAJI YA MWEZI MEI?

Ndugu Mteja, bili za Mwezi Mei zimeshatumwa kwa wateja.
Usilimbikize bili lipa kupitia njia zifuatazo:



*150*00#



*150*01#



*150*88#



*150*71#



*150*88#



www.dawasa.go.tz



Dawasatz 0800110064 BURE 0735 202121

Tafuteni vyanzo vya ziada vya fedha kuijendsha - Mha. Musira

Zamda Mabada, Kilimanjaro
na Brenda Magoma, Iringa

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imelishiauri Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) kutafuta vyanzo mbalimbali vya fedha ili kuziwezesha Kamati za Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji za Mikoa (RCCs) kupanua wigo wa kuwafikia wananchi walioko nje ya maeneo ya miji.

Ushauri huo umetolewa na Meneja wa EWURA Kanda ya Mashariki Mhandisi Nyirabu Musira alipokuwa akimwakilisha Mkurugenzi Mkuu wa EWURA wakati wa mafunzo ya kuwajengea uwezo wajumbe wa Kamati za Mikoa za Baraza (RCC) yaliyofanyika mwanzoni mwa mwaka huu mkoani Morogoro.

Mhandisi Nyirabu alisema "EWURA inatambua kazi kubwa inayofanywa na Baraza kuititia Kamati zake za Mikoa katika kuwafikia watumiaji wa huduma za nishati na maji, ndio maana imekuwa bega kwa bega kuhakikisha Baraza lin-

afikia malengo yake. Hata hivyo, kwa kuwa shughuli za Baraza zinaongezeka siku hadi siku nashauri Baraza kuendelea kutafuta vyanzo zaidi vya mapato ili kuhakikisha linafikia malengo yaliyokusudiwa."

Katika hatua nyingine, Mhandisi Musira aliliomba Baraza kuendelea kutoa ushirikiano wa kutosha kwa Kamati zake kwa utekelezaji makini wa majukumu yake.

"Endeleeni kuziwezesha Kamati zenu ili ziweze kutekeleza vyema majukumu yake ikiwemo kuelimisha watumiaji wa huduma za nishati na maji na kuelimisha watumiaji kuhusu utaratibu wa kuwasilisha malalamiko pindi wanaposhindwa kupata huduma zenye ubora," alieza Mhandisi Musira.

Aidha aliwasisitiza Wajumbe wa Kamati za mikoa za Baraza kushirikiana na Baraza katika kufikia malengo kwa kujitoa kwa dhati ili vipaumbele vya kiutendaji vya Baraza viweze kufikiwa.

Alilishauri Baraza kuyafanya mafunzo hayo ya kuwajengea uwezo Wajumbe wa Kamati kuwa endeleku ili kuendana na wakati kutokana na mambo mengi kubadilika hasa

kwenye masuala yahusuyo urekebishwaji wa kanuni mbalimbali za maji, umeme, gesi na mafuta.

"Ni vyema mafunzo haya yawe yanafanyika kila mara ili kuendana na wakati, vinginevyo mnawenza kujikuta mnatumia taarifa zilizopitwa na wakati na mkapotosha umma," alisema Mha. Musira.

Kuhusu mafunzo hayo, Mwenyekiti wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Mkoa wa Iringa, Bw. Painetho Madembwe, alisema kuwa mafunzo hayo yalikuwa mazuri na yamempa ujuzi na uzoefu zaidi kuhusu kazi za Baraza na namna ya utekelezaji wa majukumu yake.

"Mafunzo yalikuwa mazuri na yameniongezea ujuzi na uzoefu zaidi kuhusu kazi za Baraza na namna ya utekelezaji wa majukumu yake. Pia yamenihamasisha kusoma zaidi sheria, kanuni, na taratibu zilizowe-kwa," alisema Madembwe.

Akiongea na Jarida la Mtumiaji, Katibu Mtendaji wa Baraza Bi. Stella K. Lupimo alisema kuwa kifungu namba 33(1) (c) cha Sheria ya EWURA, kinatoa mamlaka kwa Baraza kutafuta vyanzo vya mapato na kwa kutumia kifungu hicho EWURA CCC imekwisha anza kulifanyia kazi sua-la la kutafuta vyanzo zaidi vya fedha ili kuongeza mapato na kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya Baraza kwa ufanisi zaidi.



Mhandisi Nyirabu Musira, Meneja wa EWURA Kanda ya Mashariki, akiwasilisha hotuba ya ufunguzi kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu EWURA wakati wa mafunzo ya Wajumbe wa Kamati za Mikoa za Baraza yaliyofanyika mapema mwaka huu, mjini Morogoro. Picha na Mpigapicha Wetu



Wateja mikoa ya Tanga na Mtwara kulipwa fidia

Nuru Zuberi, Tanga

na Emmanuel Paul, Mtwara

Mamlaka ya Udhibiti ya Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imeliamuru Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kumpatia jokofu mbili mpya kutokana na hitilafu ya umeme iliyounguza jokofu zake pamoja na kumlipa fidia ya kiasi cha shilingi 2,000,000/- mteja wake Bw. Abdulsamad Shariff Attasy mkazi wa Barabara ya 17 jijini Tanga, baada ya kuthibitika kuwa hasara hiyo iliokana na hitilafu ya msongo mdogo wa umeme.

Hukumu hiyo ilitolewa na kusomwa mnamo mwezi Mei, 2024 mbele ya pande zote mbili ambapo EWURA iliataka TANESCO kumpatia vifaa hivyo vipyta mteja wake na kumlipa fidia ya fedha kwa kumsababishia mteja mshtuko na hasara katika biashara yake ya samaki ali-yokuwa akiifanya.

Akisoma hukumu hiyo Afisa Huduma kwa Wateja wa EWURA kanda ya kaskazini Bi. Christine Martin alisema kuwa, EWURA ilisikiliza maelezo na ushahidi kuto-ka pande zote mbili na kujiridhisha

kuwa msongo mdogo wa umeme ndio uliosababisha uharibifu wa vifaa hivyo vya mteja huyo.

Kwa upande wake Bw. Abdulsamad Shariff Attasy ambaye ni mlalamikaji alioneshwa kuridhishwa na uamuhi huo ilitolewa na EWURA, na alitoa shukrani kwa EWURA CCC kwa msaada wa kielimu waliompatia hadi kufikia kufidiwa hasara aliyopata.

"Nikisema ukweli bila kiongozi huyu wa Baraza nisingekuwa na nguvu yoyote ya kujisimamia, nimefurahi sana kwani alinipa moyo na kuniongoza," alisema Bw. Attasy.

Mteja huyo wa TANESCO alimshukuru Afisa wa EWURA CCC kwa mwongozo na jitihada zake alizozionesha katika kuitafuta haki yake hadi kufikia kulipwa fidia na majokofu yake ambayo yalikuwa yameungua kutokana na hitilafu ya umeme.

Katika hatua nyingine huko mkoani Mtwara, EWURA imeliamuru Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kuliondoa deni la kiasi cha shilingi milioni tatu na laki mbili (3,200,000/-) kwa Bi. Ashura Yakub Mohamedi mkazi wa kata ya Rahaleo wilayani Mtwara.

Akisoma hukumu hiyo tarehe 12 Mei 2024 mbele ya pande zote mbili, Afisa Huduma kwa Wateja wa EWURA Kanda ya Mashariki ndugu Michael Mbaga, alisema kuwa, EWURA imejiridhisha pasina shaka kuwa deni hilo alilowekewa Bi. Ashura kwenye akaunti yake halikuwa halali kuwekwa kwenye mita yake, na hivyo TANESCO kuamuriwa kusitisha mara moja na kurejesha kiasi chote cha shilingi 568,000/- kili-chokuwa kimekwishakatwa kupitia manunuzi yake ya umeme.

Bi. Yakub alilishukuru Baraza kwa kuwa karibu na watumiaji wa huduma za nishati na maji, na kwa ushauri ambao Baraza limekuwa likiutoa kwa watumiaji juu ya kudai haki zao pindi zinapokiukwa.

Akizungumza kwa furaha baada ya hukumu hiyo, Bi. Ashura amesema "ninayo furaha kubwa na naishukuru EWURA CCC kwani isingekuwa ushauri na mwongozo wake nisingepata haki yangu hii leo."

Wasoma hukumu kutoka EWURA wote kwa nyakati tofauti walifanua kwa kusema kuwa kama kutakuwa na upande ambao haukuridhika na hukumu hiyo basi wanayo nafasi ya kukata rufaa katika Baraza la Ushindani (FCT) ndani ya siku 21 kwa mujibu wa Kanuni ya 23 ya Kanuni za EWURA za Utatuvi wa Migogoro za Mwaka 2020 na kama rufaa haitatka itatafsirika kuwa pande zote mbili zimekubaliana na hukumu hiyo.



Wajumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Rukwa, pamoja na uongozi wa Mamlaka ya Maji Safi Sumbawanga (SUWASA), wakati wa kikao rasmi cha majadiliano kuhusu huduma za maji kilichofanyika katika ofisi ya SUWASA Sumbawanga hivi karibuni. Picha na Mpigapicha Wetu

Suluhu uhaba wa maji Sumbawanga

Na Mwandishi wetu, Rukwa

Wakazi wa Manispaa ya Sumbawanga wanatarajia kuondokana na adha ya upungufu wa maji kutokana na kuanza kwa mradi wa ujenzi wa bwawa la maji lenye ujazo wa lita milioni 13 kwa siku, utakaogharimu shilingi za Kitanzania bilioni 2.6.

Mradi huo unaotegemewa kujengwa eneo la Msitu wa Mbizi (TFS) katika Manispaa ya Sumbawanga, utawanufaisha wananchi wa Manispaa hiyo pamoja na maeneo ya jirani na hivyo kuondoa kabisa kero ya uhaba wa maji hasa wakati wa kiangazi.

Hayo yamesemwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Sumbawanga (SUWASA), Mhandisi Gibon Nzowa wakati wa kikao na Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji mkoani

Rukwa (Rukwa RCC) kilichofanyika hivi karibuni katika ofisi za Mamlaka hiyo.

Katika kikao hicho ambacho ni mwendelezo wa vikao vya Kamati ya Watumiaji na SUWASA, ziliibiliwa hoja mbalimbali zikiwa na lengo la kuleta maendeleo ya huduma za maji kwa wakazi wa Manispaa ya Sumbawanga.

Akijibu swali lililoulizwa na Mwenyekiti wa Kamati hiyo Bi. Faustina Vallery kuhusu mkakati wa SUWASA katika kuhakikisha upatikanaji wa maji ya uhakika hasa kipindi cha kiangazi, Mhandisi Nzowa alisema kuwa, Mamlaka imejidhatiti kudhibiti hali ya uhaba wa maji wakati wa kiangazi kwa kujenga bwawa kubwa la maji litakalogharimu shilingi za Kitanzania bilioni 2.6.

"Ili kudhibiti hali ya uhaba wa maji kipindi cha kiangazi, SUWASA tumeshaandika andiko la mradi wa ujenzi wa bwawa eneo la Mbizi lenye ujazo

wa lita milioni 13 na tayari mradi huo umeshahakikiwa na bajeti kupidishwa, hivyo basi tunatege-meza ndani ya kipindi cha mwa-ka ujao wa fedha (2024/2025) ujenzi utaanza," alisema Mhandisi Nzowa.

Aidha Nzowa aliongeza kuwa kukauka kwa vyanzo vingi vya maji katika mkoa wa Rukwa kwa kipindi cha kiangazi imekuwa ni chanzo cha uhaba wa maji ndani ya Manispaa ya Sumbawanga kwa muda sasa na kwamba ujenzi wa bwawa hili la maji utaenda kupunguza au kuondoa kabisa uhaba wa maji kwa kipindi cha kiangazi na kuboresha huduma ya maji kwa ujumla kwani maji ya bwawa hilo yatatoshleza matumizi ya wateja wa SUWASA kwa kipindi kisichopungua miezi mitatu pasipo kutegemea chanzo kingine cha maji.

Naye Afisa Msaidizi Huduma kwa Wateja na Utawala wa EWURA CCC mkoani Rukwa Bw. Ramadhan Kakende alipongeza SUWASA kwa jithada wana-zochukua katika kukabiliana na changamoto za huduma ya maji na hasa ile ya uhaba wa maji kwa kipindi cha kiangazi ambayo imekuwa ni kero ya muda mrefu sasa.

"Niwapongeze SUWASA kwa kila hatua mnayochukua katika kukabiliana na changamoto za huduma ya maji na hasa hii ya uhaba wa maji kipindi cha kiangazi. Tumekuwa tukishirikiana, na zaidi SUWASA imekuwa tayari kuufanya kazi ushauri wa Kamati kila mara kunapokuwa na jambo linalohitaji ushirikiano wetu. Hii inaonesha namna mlivyo makini na tayari kupokea ushauri unao-jenga katika kuwahudumia wateja wenu," alisema Bw. Kakende.

Bw. Kakende alipongeza jithada za SUWASA katika kuongeza upatikanaji wa huduma za maji na kuahidi kuwa, EWURA CCC mkoani Rukwa itaendelea kutoa ushirikiano kwa Mamlaka hiyo ili kuhakikisha watumiaji wa huduma hizo wanasilizwa, wanawakilishwa, wanaelimishwa pamoja na kero zao kuhusu huduma za maji zinapatiwa ufumbuzi wa haraka na wa uhakika.



**WIZARA YA MAJI
MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI
WA MAZINGIRA IRINGA (IRUWASA)**



"Ndugu mteja hutakiwi kutoa fedha kwa mtu yeyote akufanyie malipo. Malipo yote IRUWASA yafanyike kuitia namba maalum ya malipo.

📞 0800 110 122 📱 @iruwa.sa 📱 @Iruwasa Iringa

Ushirikiano



**JE KUNA NGUZO IMEOZA AU IPO
MAZINGIRA YA KUTAKA KUANGUKA**

Tafadhalii ipige picha na tutumie kwa WhatsApp namba / Tupigie au tutumie ujumbe kwa namba **0733 788 208** huku ukionesha.

- ⌚ Kijiji/Mtaa
- ⌚ Eneo
- ⌚ Wilaya
- ⌚ Namba yako ya simu



**TANESCO MOROGORO TUTAIFIKIA NA
KUIFANYIA KAZI MARA MOJA**



www.tanesco.co.tz

#TupoKazini

Watumishi EWURA CCC wajengewa uwezo

Na Emmanuel C. Paul, Mtwara

Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) limewanoa watumishi wake kuitia mafunzo maalumu ya siku kumi ambayo yamefanyika mapema mwezi Mei 2024 katika Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TASUBA) ambayo yalikuwa na lengo la kuwajengea uwezo watumishi hao katika eneo la kuwasaidia watumiaji wa huduma za nishati na maji wakati wa vikao vya usuluhishi.

Akizungumza na watumishi kwa niaba ya Katibu Mtendaji wa Baraza wakati wa ufunguzi wa mafunzo hayo, ndugu Erasto Kishe ambaaye ni Mhasibu wa EWURA CCC alisema kuwa Baraza lina jukumu la kuwawakilisha na kuwasaidia watumiaji wa huduma za nishati na maji kujua haki na wajibu wao, na ili kutimiza azma hii watumishi wake ni lazima wajengewa uwezo mara kwa mara.

"Moja ya jukumu la Baraza katika kuongeza uelewa na maarifa katika eneo la kuwahudumia watumiaji wa huduma za nishati na maji ni kuwajengea uwezo watumishi wake kipi-

tia mafunzo mbalimbali. Tumieni fursa hii vizuri ili kujiongezea maarifa na ujuzi katika kuwahudumia watumiaji," alisema Bw. Kishe.

Kwa upande wao watumishi wajengewa uwezo zaidi ili kuboresha utendaji wao wa kazi katika kulitumikia tifa kwa kuwapa elimu muhimu watumiaji wa huduma hizi muhimu.

Akizungumza kwa niaba ya wafanyakazi waliohudhuria mafunzo hayo, ndugu Amani Mbogo kutoka ofisi ya Baraza mkoani Dodoma alieleza kuwa yeye na wenzake wamenufaika sana kupata mafunzo hayo yaliyolenga kuwapatia mbinu mbalimbali za kushugulikia malamalikyo ya watumiaji wa huduma za nishati na maji.

"Tunahudumia wateja wa aina mbalimbali, wakiwemo wasiojua haki zao za msingi na wengine wamepata uzoefu wa kuumiza au kuvunja moyo katika huduma za nishati na maji, hivyo ni muhimu kujua mbinu mbalimbali za kuwahudumia. Kuitia mafunzo haya tumenufaika kujifunza mbinu hizo, pamoja na masuala mtambuka katika kuhudumia wateja wetu," alisema Bw. Mbogo.

Aliongeza kuwa, kitendo cha watumishi kupewa mafunzo kwa kukanishwa pamoja kinatoa pia fursa ya kubadilishana mawazo na uzoefu juu ya changamoto mbalimbali wanazokabiliana nazo watumiaji wa huduma za nishati na maji na hivyo kujengeana uelewa juu ya mbinu za kuwasaidia.

Dkt. Kanua Juma Masaba, aliyekuwa mwezeshaji wa mafunzo hayo kutoka Taasisi ya Economic Diplomacy Consultancy alimpongeza Katibu Mtendaji wa Baraza Bi. Stella Lupimo kwa uamuvi wa kuwapatia mafunzo wafanyakazi wake kwani elimu na mafunzo ndiyo silaha kubwa ya kutekeleza malengo ya taasisi.

"Ni muhimu sana kuwapa wafanyakazi mafunzo ya mara kwa mara, kwani kwa kufanya hivyo inasaidia kuwapa ujuzi mpya na kuendana na mahitaji ya wakati husika katika utoaji huduma. Mafunzo pia husaidia kuongeza morali katika utendaji wa kazi," alipongeza Dkt. Masaba.

Alisema ni muhimu kwa wafanyakazi kupata mafunzo kwani teknolojia katika dunia inayobadilika mara kwa mara hivyo ni vyema wafanyakazi nao kuendana na mabadiliko ya maarifa na teknolojia mpya.



Bwana Lucas Jackson, Mkunzi kutoka Taasisi ya Economic Diplomacy Training Academy, akitoa mada mbele ya wafanyakazi wa EWURA CCC walipohudhuria mafunzo ya kujengewa uwezo kuhusu wa utatuvi wa migogoro na kushugulikia malamalikyo yaliyofanyika katika Chuo cha TASUBA, hivi karibuni, mjini Bagamoyo. Picha na Mpigapicha Wetu



JE, UMELIPA BILI YAKO YA YA MAJI YA MWEZI APRIL?

Ndugu Mteja, Usilimbikize bili, lipa sasa bili ya mwezi April
kupitia njia zifuatazo



www.mtuwasa.go.tz



BURE
0677 022 557
0800112160



[@mtuwasa_maji](https://www.instagram.com/mtuwasa_maji)

MTUWASA toeni elimu

Na Emmanuel C. Paul, Mtwara

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mzingira Mtwara (MTUWASA) imekumbushwa wajibu wake wa kutoa elimu kwa wadau wake wakiwemo watoto na aki na mama ili kujenga jamii ya watumiaji wenye uelewa wa huduma zinazotolewa na Mamlaka hiyo, susan juu ya namna mita za maji zinavyosomwa na bili zinavyoandaliwa.

Hayo yamesemwa na Mkurugenzi wa taasisi isiyokuwa ya kiserikali ya FB Empewernent Bi. Eva Urio katika maadhimisho ya siku ya Mtoto wa Afrika yaliyofanya katika kata ya Chuno mapema mwezi Juni, 2024, ambapo Baraza lilishiriki.

Katina maadhimisho hayo am-bayo waliwaleta Pamoja washiriki wapatao 300 wakiwemo watoto kutoka Manispaa ya Mji wa Mtwara Mikindani na viunga vyake, Bi. Urio alizungumzia umuhimu wa MTUWASA kutoa elimu kwa wateja wake ikiwemo masuala ya usomaji wa mita za maji na uandaaji wa ankara za kila mwezi.

"Ni muhimu kwa MTUWASA

kuwaelimisha wadau wake kuhusu masuala mbalimbali ya msingi juu ya huduma za maji. Mathalan kwa kundi la watoto, japojuwa ni haki yao kupata elimu kwa ujumla ni lazima pia pawepo na juhudzi za makusudi kuwajengea uelewa kuhusu huduma za maji tangu wakiwa wadogo kwa kuwa maji ni rasilimali muhimu katika maisha yao na uendeshaji wa shughuli za kiuchumi," alisema Bi. Urio.

Aidha, Bi. Urio alilitaka MTUWASA kuweka mipango ya makusudi ya kutoa elimu kwa makundi ya wateja wake, pasipo kusahau watoto katika shule wanazosoma.

Nao watoto waliohudhuria maadhimisho hayo walimshukuru Mkurugenzi huyo kwa kutambua umuhimu wao katika jamii na kwamba wanahitaji kutendewa yaliyo mema ili wawewe kukua wakiwa na mchango chanya kwa jamii yao.

Akiongea kwa niaba ya watoto wenzake, Zuhaira Mohamedi alisema kuwa wamefurahishwa na elimu waliyopewa na kuifanya siku ya Mtoto wa Afrika ioneckane ni muhimu na bora kwao kwa namna walivyothaminiwa na jamii yao.

"Tunamshukuru Mkurugenzi

wa FB Empowerment kwa kuan-daa siku hii na kuonesha thamani yetu sisi watoto. Hakika mambo mazuri tuliojifunza tutayakumbuka na kuwaeleza marafiki zetu pia. Tunashukuru pia kwa elimu ya umuhimu wa sisi kufundishwa kuhusu matumizi mazuri ya maji," alisema mtoto Zuhaira.

Akitoa salamu za kumbukumbu ya maadhimisho hayo ya Mtoto wa Afrika, Meneja Biashara na Mauzo wa MTUWASA Bi. Judith Namwele-mi alimshukuru Bi. Urio kwa kuwakumbusha kuhusu utoaji wa elimu kwa wateja wao jambo ambalo ni muhimu katika utoaji wa huduma zake.

"Tumepokea kwa mikono mi-wili ushauri wa Mkurugenzi kwani unatukumbusha jukumu letu muhimu la kutoa elimu kwa wadau wetu, na hivyo tunaahidi kuufanya kazi katika utendaji wetu," alisema Bi. Namwelemi.

EWURA CCC Mtwara hushiri-ki katika masuala mbalimbali ya kijamii ikiwemo maadhimisho mbalimbali, hii ikiwa ni sehemu ya kuongeza kujulikana kwake mion-goni mwa jamii.

Ushauri

HabariPicha



Mwenyekiti wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Mkoa wa Iringa ndugu Painetho Madembwe (kulilia) akikabidhi cheti hivi karibuni kwa Mtangazaji wa Shamba FM iliyopo mjini Iringa, Bw. Laurin Deogratius. Cheti hicho kimetolewa na Baraza kuthamini mchango wa Radio hiyo katika kulitangaza Baraza. Picha Brenda Magoma



Sehemu ya washiriki katika mku الوا wananchi uliofanyika katika Kata ya Tambukareli, Manispaa ya Tabora, mwezi Mei, 2024. Picha zote na Mpigapicha Wetu



Ndugu William Luanda, Mjumbe wa Kamati ya Watumiaji Mkoa wa Kilimanjaro akielimisha wanafunzi wa Shule ya Sekondari Reginald Mengi, kuhusu ya umuhimu wa kupima uzito wa mitungu wa gesi ya kupikia majumbani. Picha zote na Mpigapicha Wetu

HabariPicha



Afisa Utawala wa EWURA CCC, Bi. Josephine Ntaumenya akiwasilisha mada kuhusu maadili kazini wakati wa mafunzo ya kuwajengea uwezo Wajumbe wa Kamati za Mikoa za Baraza yaliyofanyika mjini Morogoro.. Picha na Mpigapicha Wetu



Wajumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Mkao wa Singida, katika picha ya pamoa na Meneja wa TANESCO Mkao wa Singida Mha. Mwamyita Ally (katikati) baada ya kikao kilichofanyika katika Ofisi za TANESCO, kujadili changamoto mbambali zinazohusu huduma ya umeme, Juni, 2024. Picha na Evarist Lucas



Mwenyekiti wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Mkao wa kikazi Ubungo, ndugu Silas Adinan Sued akieleza haki na wajibu wa mtumiaji wa huduma za nishati na maji kwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Maji kilichopo Ubungo, mwezi Juni, 2024. Picha na Catherine Ochido



WIZARA YA MAJI
MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI
WA MAZINGIRA IRINGA (IRUWASA)

TUMEFIKIA 97%
97% ya wakazi wa Manispaa ya Iringa
wanafurahia huduma ya maji safi na salama

www.iruwasa.go.tz More info 0800 110 122 

 @Iruwa.sa

Fahamu umuhimu wa kutafuta taarifa sahihi za huduma za nishati na maji

Na Ramadhan Kakende, Rukwa

Wanazuoni husema taarifa ni chanzo cha nguvu ya uelewa, na ni chanzo cha maarifa. Ukiwa na taarifa sahihi ni vigumu kudanganywa au hata kuonewa kwenye jambo lolote linalokuhusu au ulilo na maslahi nalo.

Kama mwanadamu ambaye unazungukwa na mambo mengi yakiwemo ya kijamii, kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni, ni muhimu kuwa na taarifa sahihi wakati wote kwani mambo hubadilika mara kwa mara.

Hivyo hivyo katika huduma za nishati na maji ni muhimu kuwa na taarifa sahihi wakati wote ili kupata huduma zilizo bora na uweze kufaidika nazo. Huduma hizo ni pamoja na maji, umeme, mafuta yatokanayo na petroli pamoja na gesi ya kupikia majumbani (LPG).

Kwenye makala hii mwandishi anaeleza umuhimu wa kutafuta taarifa sahihi kuhusu huduma za nishati na maji kama mtumiaji wa huduma hizo.

Kutambua haki na wajibu

Kwa kutafuta taarifa sahihi kwa kušoma au kusikiliza vyombo vya habari, itakuwezesha kufahamu haki na wajibu wako kama mtumiaji wa huduma za nishati na maji, na hivyo kujihami dhidi ya kudanganywa au kupoteza haki zako za msingi.

Kujiamini zaidi anapotumia huduma

Taarifa sahihi zinamwongezea mtu kujiamini kwa kuwa anakuwa anafahamu ni hatua zipi anapaswa kuchukua kulingana na mahitaji ya wakati huo kuhusu huduma husika. Hii inawezesha kuhoji au kutaka kufahamishwa zaidi na mtoe huduma kuhusu taarifa muhimu anayopswa kuipata.

Kufahamu njia sahihi za kuwasilisha malalamiko

Kuwa na taarifa sahihi juu ya huduma unazotumia itakupelekea kulalamika kwa mtoe huduma kwa njia iliyo sahihi ikiwemo kufuata taratibu za kuwasilisha malalamiko. Kutokuwa na taarifa sahihi kunaweza kusababisha mtu apoteze haki zake ambako kunaweza kusababishwa na

uwasilishaji wa malalamiko nje ya muda uliowekwa kisheria.

Chachu ya mtoe huduma kuboresha huduma zake

Endapo kuna uelewa mkubwa mionganoni mwa watumiaji wa huduma za nishati na maji kutafanya watoe huduma waboreshe huduma zao kwa kuwa watumiaji watadai huduma bora. Jamii kubwa ya watumiaji wa huduma kuwa na taarifa sahihi pia kunawezesha uwajibikaji kwa pande zote mbili, yaani mtoe huduma na mteja. Kila mmoja atajua wajibu wake kisheria na haki zake pia.

Kuwa na mipango bora ya matumizi

Mtumiaji anaweza kupanga matumizi yake kulingana na taarifa zilizopo, kama vile wakati ambao kuna katizo au uhaba wa huduma, gharama za huduma n.k, hivyo katumia huduma kwa uangalifu mkubwa. Kwa ujumla, kuwa na taarifa sahihi kunawezesha mtumiaji kutumia huduma za nishati na maji kutumia huduma hizo kwa namna bora zaidi huku akizingatia masuala yote ya kiu-chumi, kimaadili na kimazingira.

Kamati ya watumiaji Kagera yapewa somo

Na Anadorice Komba, Kagera

Wajumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Mkoa wa Kagera, hivi karibuni wamenufaika na elimu kuhusu matumizi sahihi ya gesi za kupikia majumbani.

Elimu ilitolewa na Kampuni ya Lake Gas ambapo wakati wa ziara ya Wajumbe iliyofanyika kwenye ofisi za Kampuni hiyo.

Akitoa elimu hiyo, Meneja Masoko wa Lake Gas mkoaa wa Kagera Bw. David Shaban alisema kuwa, shida kubwa iliyopo kwa watumiaji wa gesi ya kupikia ni mazoea na kumpungua kwa umakini wa matumizi ya gesi kadiri wanavyozoea kutumia nishati hiyo ya kupikia.

"Wateja wengi huwa na umakini mwanzoni wanapoanza kutumia gesi, lakini wakizoe tu umakini hupungua kwa kiwango kikubwa," alieleza ndugu Shaban na kuongeza kuwa "kuna wakati 'valvu-raba' au 'horsepipe' katika mtungi huwa inalega hali ambayo husababisha uvu-

jaji wa gesi. Hata hivyo cha kusikitisha ni kwamba kuna baadhi ya watumiaji huchukua jiwe na kuweka juu ya 'regulator' ya gesi, jambo ambalo humweka mtumiaji katika hatari ya mlipuko wa moto."

Aliwaasa watumiaji kuchunguza mitungi ya gesi kabla na baada ya kupika na ili kubaini changamoto yoyote ya uvujaji na kuweza kuishugulikia.

"Ukichunguza mtungi wako utasaidia kugundua mapema kama kuna shida kwa sababu katika gesi za kupikia (LPG) zimewekewa 'Sulphur' ambayo harufu yake inamsaidia mtumiaji kugundua kwa urahisi na kwa wakati kama kuna uvujaji wa gesi, na hii inasaidia kuepusha majanga ya moto yanayoweza

Wajumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Mkoa wa Kagera, katika picha ya pamoja na wafanyakazi wa Kampuni ya Lake Gesi wakati Kamati ilipotembelea ofisi ya Kampuni hiyo ya uuzaaji wa gesi ya kupikia kwa ajili ya kujifunza namna inavyowahudumia wateja wake.

Picha na Anadorice Komba



kusababishwa na uvujaji wa gesi," alisisitiza Meneja huyo.

Akizungumza baada ya ziara hiyo, Katibu wa Kamati ya Watumiaji ya Mkoa wa Kagera ndugu Eustadi Katunzi, alishukuru Lake Gas kwa kufanikisha ziara hiyo, na kwa kutoa elimu muhimu kuhusu gesi za majumbani.

Katunzi alisema kupitia ziara hiyo, wajumbe wa Kamati wamenufaika kwa kupata elimu kuhusu mambo mbalimbali yanayohusu gesi ya kupikia majumbani ikiwa ni pamoja na namna ya kudhibiti viashiria vinavyoweza kusababisha gesi kuvuja na pengine kuleta majanga ya moto.

Sambamba na hilo, ndugu Katunzi alieleza kuwa, ziara hiyo imewanufaisha Wajumbe wa Kamati hiyo kwa kujifunza juu ya matumizi sahihi ya majiko ya gesi za kupikia.

"Kupitia ziara hii tumejifunza kuhusu taratibu za kuzima jiko baada ya kupikia ambapo taratibu hizo huenda sambamba na kuzima mtungi. Kwa kuwa mara nyingi sisi watumiaji huwa tunazima jiko tu na kusahau kuzima gesi kwenye mtungi, ikitokea gesi imevuja na ukawasha jiko lazima kutatokea mlipuko hivyo ni muhimu sana kwetu sisi watumiaji wa gesi baada ya kumaliza kupika tuzime jiko pamoja na upande wa mtungi," alisema Katunzi.

Naye Mwenyekiti wa Kamati hiyo Bw. Najim Bwanika alisema awali hakuwa anajua kama mpira (horsepipe) inatakiwa kubadilishwa kila baada ya miezi sita lakini kupitia ziara hiyo amepata kupata uelewa huo.

"Tunaomba elimu hii isiishie kwetu tu bali pale tutakapo andaa programu za uelimishaji kwa jamii tunawaomba nanyi kutupatia mtaalamu kuja kushiriki ili elimu hii isambae kwa kwa watumiaji wengi zaidi sababu watu wengi wanatumia gesi za majumbani pasipo kufahamu nini wanatakiwa kufanya na kipi hawat-akiwi kufanya," alisema Bwanika.

Kamati ya Watumiaji mkoani Kagera itaendelea kukutana na watoa huduma wa huduma zinazodhibitiwa na EWURA kwa nia ya kujifunza na kujenga mahusiano mazuri na watoa huduma hao ili watumiaji wapate huduma wanazostahili, zenyne ubora na bila kupata madhara.

Uelimishaji

Walalamikia maji machafu wakati wa mvua kubwa



Na Neema Nnko, Manyara

Wakazi wa Babati mjini wamelalamikia tatizo la kupata huduma ya maji machafu hasa wakati wa mvua, kitendo ambacho kinawapa hofu ya kupata madhara ya kiafya.

Wakieleza kuhusu hali hiyo wakati wa programu za uelemishaji katika vikundi vya watu mbalimbali ikiwemo vijiwe vya kahawa zilizofanywa na EWURA CCC Mkoa wa Manyara, wakazi hao wameeleza wasiwasi walionao juu ya afya zao kutokana na maji machafu wanayotumia.

Akielezea kuhusu hali hiyo ndugu Venance Masingi, mkazi wa eneo la Mrara mjini Babati alisema "tunaelewa kuwa wakati mvua zin-

aponyesha changamoto nyingi hujitokeza, lakini hali hii ya ubora wa maji hairidhiishi. Tunakunywa na kupikia maji machafu yenye rangi, jambo linaloleta hofu ya kupata magonjwa."

Kwa upande wake ndugu Antipasi Menei mkazi wa Osterbay ameeleza kusikitishwa kwake na hali ya maji kwani si salama kwa matumizi ya kunywa na kupikia, jambo linalompa wasiwasi na kuingia gharama ya zida ya kutafuta maji sehemu nyingine kwa matumizi ya kupikia na kunywa.

"Nashindwa kuyaamini maji tunayopata kutoka kwenye chanzo chetu kwa matumizi ya kupikia na kunywa hivyo kulazimika kutafuta maji kutoka maeneo mengine tofauti kwa matumizi ya

Picha ikioneshaa
maji machafu
ambayo wananchi
wa baadhi ya
maeneo ya
maji wa Babati
waliyalalamikia.
Picha na Neema
Nnko

nyumbani," ameeleza ndugu Menei.

Mzee Augustino Hizza ni mionganoni mwa watu waliopaza sauti zao huku akiiomba Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Babati (BAWASA) kuchukua hatua stahiki ili kuondokana na adha hiyo ya maji machafu, huku akisisitiza kuwa kupata huduma bora ya maji safi na salama ni haki ya watumiaji.

"Nawasihi BAWASA kuchukua hatua stahiki na haraka wakati wa mvua ili kuifadhi maji na kuyasambaza kwa wateja kwa usalama ili kuondoa adha hii ya kutumia maji machafu," alisema Hizza.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa BAWASA Mhandisi Idd Msuya, alikiri kupokea malalamikio hayo huku akiileza kuwa BAWASA ina mikakati ya muda mrefu ya kuwa na matanki ya kuifadhi maji hivyo kutowalazimu wao kusukuma maji wakati wa mvua kubwa moja kwa moja kwa wateja.

Mhandisi Msuya alisema wakati wa mvua mabomba huwa na tabia ya kuvuta uchafu kwenye njia na kusababisha uchafu kuingia kwenye maji na kuongeza kuwa kwa sasa BAWASA inafanya jitihada za kulinda vyanzo vya maji na ikitokea mvua kubwa watasitisha kusukuma maji kwa wakati huo kuepuka adha hiyo.

EWURA CCC Mkoa wa Manyara itaendelea kutoa elimu na kusaidia wananchi kutatua kero zao juu ya huduma za nishati na maji kwani bado wananchi wanahitaji huduma hii ili waendelee kuelewa wajibu wao lakini pia wawe na tabia ya kulalamika na siyo kunung'unika wakiwa majumbani mwao.



Fuateni ratiba ya mgao wa maji kikamilifu - Mhe. Komba

Na Mwandishi wetu, Geita

Mkuu wa Wilaya ya Geita Mhe. Hashimu Komba ameiasa Mam-laka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Geita (GEU-WASA) kufuata kikamilifu ratiba ya mgao wa maji kwa wananchi wa halmashauri ya mji wa Geita na viunga vyake.

Akiongea kwenye kikao maalumu cha wadau wa maji kilichoketi hivi karibuni na kuhudhuriwa na wafanyakazi wa RUWASA, GEUWASA, EWURA CCC pamoja na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Geita, Mkuu huyo wa Wilaya alieleza umuhimu wa Mamlaka kufuata ratiba ya mgawo ili kupunguza changamoto za upatikanaji wa maji mionganoni mwa wateja wa Mamlaka hiyo.

"Pamoja na uwepo wa mgao wa maji kutokana na kutokutosheleza mahitaji ya watumiaji wote kwa wakati mmoja, ni muhimu kwa GEUWASA kufuata ratiba ya

mgao huo ambayo mmeitoa wenye. Kwa mfano ikiwa siku ya Jumatano ni siku ya kuelekeza maji katika mtaa fulani ni vyema siku hiyo maji yapatikane katika mtaa huo," alisisitiza Mkuu huyo wa Wilaya.

Alisema alilazimika kuitisha kikao hicho maalumu cha wadau wa maji kutokana na manung'uniko anayoyapata mara kadhaa kwenye mikutano ya wananchi juu ya kuto-fuatwa kwa ratiba ya mgao wa maji Geita mjini, na kwamba kuna baadhi ya maeneo kama-vile Nyankumbu na Nyantoro-toro hupata maji mara mbili tu kwa wiki.

Akitolea ufanuzi kuhusu suala hilo Mkurugenzi Mtendaji wa GEUWASA, Mhandisi Frank Changawa alielezea kwamba, kuna changamoto ya usambazaji wa maji kwani uzalishaji ni mdo-go kuliko mahitaji.

"Ninakiri kwamba kiwango chetu cha uzalishaji wa maji ni kidogo kuliko mahitaji ya wananchi wa Geita mji,"

alisema Mhandisi Changawa na kuongeza kuwa, GEUWASA inaendelea kufanya mipango ya muda mfupi na muda mrefu ili kuongeza uzalishaji wa maji ili kuondokana na changamoto hiyo ya mgao wa maji.

Akichangia hoja kwenye mkutano huo Mwenyekiti wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji mkoa wa Geita Ndugu Dot-to Paul alisema kuwa, Kamati hiyo imekuwa ikipata malalamiko mara kadhaa kutoka kwa wananchi kuhusu kutofuatwa kwa ratiba ya mgao wa maji ambayo imewekwa na GEUWASA wenye.

Bw. Paul aliitaka GEUWA-SA kufuata ratiba ya mgao ili watumiaji wajipange ni kwa namna gani watatumia maji kwa kipindi chote cha mgao.

Aidha aliitaka GEUWA-SA kuhakikisha ina mipango thabiti ya kudhibiti maji yanayopotea ili maji yote yanayozalishwa yanufaishe watumiaji wengi zaidi.

Mkuu wa Wilaya ya Geita ndugu Hashimu Komba akitoa maelekezo kwa uongozi wa GEUWASA kuhusu umuhimu wa kuzingatia ratiba ya mgao wa maji kwa wakazi wa Geita wanaotegemea chanzo cha maji cha Nyamkanga. Picha na Mpigapicha Wetu

Wahoji suluhisho la mgao wa maji

Na Chiipegwa Samwel, Morogoro

Wanaklabu wa EWURA CCC Shule ya Sekondari Kingalu Manispaa ya Morogoro wamehoji sababu za uwepo wa mgao ya maji katika Manispaa hiyo huku wakitaka kujua suluhisho lake ili watumiaji wasipate kadhia hiyo ambayo imekuwa ikiwasumbua kwa muda mrefu.

Hoja hiyo imekuwa wakati wa ziara ya wanaklabu hao kwenye chanzo kikuu cha maji cha Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA) waliyoifanya kwa lengo la kujifunza mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kujua namna Mamlaka hiyo inavyofanya shughuli zake za kusambaza huduma ya majisafi kwa wateja.

Akiongea wakati wa ziara hiyo, Yusuph Juma mmoja wa wanaklabu wa EWURA CCC Shule ya Sekondari Kingalu alitaka kujua ni namna gani MORUWASA wanaweza kuongeza ukubwa wa bwawa hilo ili kukidhi mahitaji na kuondoa mgao wa maji.

"Ninatamani kufahamu ni kwa namna gani bwawa hili la Mindulinaweza kuongezwa ukubwa ili kuhifadhi maji mengi zaidi na hatimaye kuhudumia watu wengi zaidi ndani ya Manispaa ya Morogoro na

hivyo kupunguza mgao wa maji," aliliza Juma.

Akijibu hoja hiyo Afisa Haidrolloja wa MORUWASA ndugu Yohana Mwaigaga aliwaeleza wanaklabu hao kuwa, ukubwa wa bwawa hurekebishwa kwa kuongeza kina chake na tuta ambapo ikifanyika hivyo maji yatapatikana mengi na kupunguza mgao kwa watumiaji wa huduma hiyo.

Mwaigaga alisema kuwa "Kwa sasa MORUWASA tumeshaandaa mpango wa kutekeleza mradi wa kuongeza kina katika bwawa hilo na kujenga mtambo mkubwa wa kutibu maji, hivyo mradi huo ukitekeleza changamoto ya mgao wa maji ndani ya Manispaa ya Morogoro itapungua kama siyo kuisha kabisa."

Aidha ndugu Mwaigaga alieleza kuwa shughuli za kibinadamu kama vile ukataji na uchomaji miti iliyo pembezoni mwa Bwawa, shughuli za kilimo ambacho si rafiki kwa bwawa, uvuvi haramu na mabadiliko ya kimazingira zimekuwa ni changamoto kubwa zinazothirisho chanzo hicho cha maji.

"Katika kukabiliana na changamoto nilizozitaja MORUWASA tunachukua hatua mbalimbali ikiwa ni Pamoja na kuweka ulinzi kwenye chanzo hiki, kuhamasisha

jamii kutokukata miti hovskyo, na kutoa elimu ya kulinda vyanzo ya maji. Ninaamini kuwa kuititia jitihadi hizi tunazofanya zitasaidia kulifanya bwawa kutokupungua kina na hivyo kuwa na maji mengi ambayo yatapunguza mgao wa maji kwa watumiaji."

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Klabu ya EWURA CCC Shule ya Sekondari Kingalu Bw. Richard Cornel, aliwashukuru wataalamu wa MORUWASA kwa maelezo na mafunzo waliiyowapa wanaklabu kuhusu huduma ya maji wakati wa ziara hiyo.

"Tunapenda kushukuru uongozi mzima wa MORUWASA kwa kukubali ombi letu la kuja kuwatembelea na kujifunza namna mnavyoyachakata maji hadi kutufikia walaji, lakini pia mmekata kiu yetu ya maswali mbalimbali ambayo hatukuwa na majibu ya kitaalamu. Tunawaahidi tutakuwa mabalozi wenu wa kuwaelimisha wanafunzi wengine, wazazi na walezi juu ya umuhimu wa kutunza vyanzo ya maji na namna mnavyohakikisha ubora wa maji kabla ya kumfikia mlaji," alisema Cornel.

EWURA CCC ilianzisha Klabu za Wanafunzi kwenye shule za msingi na sekondari ikiwa ni mkakati mahususi wa kuyafikia makundi rika ya vijana na kuweka wepesi wa kuelimisha makundi hayo, ili kuwaandaa kuwa watumiaji wenye kuchangia maboresho ya huduma za nishati na maji nichini.



Miongoni mwa wanafunzi wa Klabu ya EWURA CCC Shule ya Sekondari Kingalu, Manispaa ya Morogoro wakifuatilia kwa ukaribu maelezo ya hatua za kutibu maji katika mtambo wa kutibu maji wa MORUWASA, Mafiga Morogoro. Picha na Chiipegwa Samwel



Fahamu faida za ripoti za utendaji wa mamlaka za maji zitolewazo na EWURA

Na Sakina Yusuf, Tabora

Sifahamu kama kuna ripoti za utendaji wa mamlaka za maji ambazo hutolewa na EWURA.
Hata hivyo, kwa siku za hivi karibuni nimekuwa nikiona mabadi-liko chanya makubwa kwa Mamlaka yetu ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tabora (TUWASA) yanayoashiria kuboreshwa kwa huduma.

Haya ni maneno ya Bw. Saidi Chetemo mkazi wa Kidatu katika Manispaa ya Tabora aliyoyasema baada ya kutembelea ofisi ya EWURA CCC mkoani Tabora, ambapo alipatiwa elimu kuhusu kazi za Baraza na kupatiwa nakala ya taarifa ya utendaji wa mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira 2022/23 kutoka EWURA.

Kwa mujibu wa kifungu cha 29(2) cha Sheria ya Maji na Usafi wa Mazingira Sura namba 272, EWURA hutoa taarifa za utendaji za mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira nchini.

"Kwa miaka 15 mfululizo, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imekuwa ikiandaa taarifa za mwaka za utendaji wa mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira Tanzania bara.

"Madhumuni ya taarifa hizo ni kuujulisha umma kuhusu hatua ili-yofikiwa na mamlaka za maji katika kutoa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira, kupima jitihada za mamlaka hizo katika kufikia malengo ya utendaji kazi na kupendekeza hatua za kuboresha utoaji wa huduma,

inasema sehemu ya Muhutasari wa Taarifa ya Utendaji wa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2022/23.

Mbali na umuhimu wa ripoti hizi, watumiaji wa huduma za maji bado wana uelewa mdogo kuhusiana na taarifa zilizomo katika ripoti hizi, ama kwa kutofahamu uwepo wake au kwa kutokutafuta taarifa kuhusu ripoti hizi.

Ripoti za utendaji wa mamlaka za maji zina umuhimu mkubwa kwa watumiaji wa huduma za maji katika kuboresha huduma za majisafi na usafi wa mazingira nchini. Makala hii itazungumzia faida chache kwa watumiaji wa huduma za maji zinazokusudiwa na ripoti hizi:-

Kushirikisha Watumiaji

Ripoti hizi zinatoa fursa kwa wananchi kushiriki katika mchakato wa ufuatiliaji na kutoa tathmini ya huduma za maji katika maeneo wanayoishi. Hii inahamasisha ushirikiano kati ya mamlaka za maji na watumiaji hivyo kurahisisha mchakato mzima wa kuboresha huduma.

Kupokea Taarifa Sahihi

Watumiaji kuitia ripoti ya utendaji wa mamlaka za maji nchini wanapata taarifa sahihi kuhusu hali ya huduma za maji, ikiwemo upatikanaji, ubora, na gharama za miradi ya maji. Hii itawawezesha kufanya maamuzi sahihi kuhusu matumizi ya maji na huduma zinazohusiana na rasilimali hiyo.

Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Mha. Mwajuma Waziri, akionesa Ripoti ya Utendaji kazi wa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira kwa mwaka wa fedha 2022/2023, mara baada ya kuzindua Ripoti hiyo, Machi 2024, jijini Dodoma. Picha kwa hisani ya tovuti ya Mzalendo

Kuboresha Huduma

Ripoti hizi ni chachu ya uboreshwaji wa huduma za maji na hivyo watumiaji wataweza kupata huduma bora kwani mamlaka za maji hufanya maboresho ya huduma katika maeneo yenye changamoto yaliyoainishwa katika ripoti hizo hivyo kupelekeea kuimarisha upatikanaji wa huduma bora za maji kwa watumiaji. Uelewa wa watumiaji wa ripoti hizo hutengeneza msukumo mkubwa kwa mtoa huduma kufanya maboresho.

Uwajibikaji na Uwazi

Ripoti hizi husaidia mamlaka za maji kuwa wa wazi na kuwajibika kwa watumiaji wa huduma kuhusu jinsi wanavyotoa huduma za maji na usafi wa mazingira. Pia inawapa watumiaji uelewa wa jinsi fedha zao zinavyotumika na kuwekeza katika miradi ya maji, udhibiti wa upotevu wa maji na ubora wa huduma wanazopokea kutoka kwa mamlaka. Ikiwa watumiaji watafahamu taarifa hizo, wanaweza kuhoji mwenendo wa utoaji huduma kutoka katika mamlaka za maji husika katika maeneo yao

Kutokana na umuhimu wa ripoti hizo, Baraza linawahimiza watumiaji kutafuta taarifa hizo si tu kwa ajili ya kujua utendaji wa mamlaka za maji katika maeneo yao bali pia kuwa sehemu ya kuboresha huduma hizo kwa kushauri na kutoa maoni pindi wanapohitaji kufanya hivyo. Taarifa hizo zitawapatia uelewa na kutoa msukumo kwa mamlaka kufanya maboresho yenye tija katika huduma.

Fahamu nafasi ya EWURA CCC, utekelezaji wa Misingi ya Sera ya Maji, 2002

Na Neema Nnko, Manyara

Shemu ya III ya Sera ya Maji ya mwaka 2002 inazungumzia kuhusu huduma ya majisafi na majitaka. Sera hiyo inaeleza kuwa madhumuni yake ni kuwezesha uendelezaji na usimamizi endelevu wa utoaji wa huduma

ya majisafi na uondoaji majitaka kwa wakazi wa mijini.

Sera inaeleza pia kuwa madhumuni hayo yatafikiwa kwa kuweka malengo na kutoa miongozo na vigezo vya utekelezaji wa shughuli zinazofanywa na Mamlaka za Majisafi na Majitaka Mijini na watekelezaji wengine, kwa nia ya

kuboresha huduma ya utoaji majisafi na uondoaji majitaka mijini.

EWURA CCC kwa upande wake imejidhatiti katika kutoa mchango wake wakati wa utekelezaji wa Sera katika eneo la kutoa elimu kwa watumiaji wa hudumza za maji ili wailewe Sera hii. Katika Makala hii, Baraza linaleta kwako Sera hii



JE? wajua

Sababu zinazopeleka Bili kubwa za Maji?

- ▲ Matumizi ya maji yasiyo sahihi
- ▲ Mvujo mbele ya Dira (Mita)
- ▲ Usomaji wa mita usiyo sahihi
- ▲ Tatizo la Dira

Kwa lalamiko la bili kubwa tafadhali wasiliana nasi kwa namba 0800751011 (BURE)

au 0736 737736 WhatsApp tu
au fika katika ofisi zetu Mara tu
upatapo usomaji wa Dira yako au bili yako



kwenye upande wa huduma ya majisafi na uondoaji majitaka mijini, ambapo imejengeka katika misingi ifuatayo:-

1. Haki ya Kila Mwananchi

Majisafi na Usafi wa Mazingira ni muhimu kwa maendeleo na hivyo ni haki ya kila mwananchi kupatiwa huduma hizi. Ni jukumu la Serikali na Mamlaka husika kuhakikisha upatikanaji wa majisafi kwa wananchi wote. Msingi huu unaendana na haki ya kupata huduma ya msingi ambayo Baraza linahamasisha katika program zake za uelimishaji.

2. Udhibiti wa Ubora wa Huduma

Ubora wa huduma zitolewazo ni muhimu. Huduma za majisafi na uondoaji majitaka zinapaswa kufikia viwango vya juu vya ubora ili kuhakikisha afya na usalama wa watumiaji. Msingi huu unaenda sambamba na haki ya usalama wa huduma ambayo ni mionganini mwa haki nane za mtumiaji wa huduma.

3. Ulagizima wa Kulipia Huduma

Ulipiaji gharama zote za utoaji na uendelezaji wa huduma ya majisafi na uondoaji majitaka mi-

“ **Ni wajibu** wa wakazi wote mijini kulipia gharama zote za kuondoa na kusafisha majitaka wanayozalisha kulingana na kiasi cha maji wanayotumia

jini ndio mhimiili mkuu wa kuhakikisha kuwa huduma hii inakuwa endelevu. Hii inamaanisha wakazi wanapaswa kulipia huduma hizi ili kuhakikisha zinaendelea kutolewa kwa ubora na ufanisi. Huu ni moja wa wajibu wa msingi wa watumiaji wa huduma za maji uwajibikaji.

4. Wajibu wa Wakazi Kulipia Gharama za Majitaka

Ni wajibu wa wakazi wote mijini kulipia gharama zote za kuondoa na kusafisha majitaka wanayozalisha kulingana na kiasi cha maji wanayotumia. Hii ni muhimu ili kudumisha usafi wa mazingira na afya ya umma.

5. Kudhibiti Matumizi ya Maji

Msisitizo mkubwa utawekwa kwenye kudhibiti matumizi ya maji na kuzuia upotetu. Hii ni pamoja na kuhamasisha matumizi ya teknolojia za kuokoa maji na kuelimisha wananchi kuhusu matumizi sahihi ya maji. Hili ni moja ya maeneo muhimu yanayozingatiwa katika program za uelimishaji za Baraza.

6. Kuweka Mipango kwa Wakazi Wenye Kipato Kidogo

Wakazi wenye kipato kidogo mijini watafikiriwa wakati wa kuweka mtandao wa kusambaza maji na kupanga bei za maji. Hii itahakikisha kuwa huduma za maji zinapatikana kwa wote bila kujali kipato chao. Hili ni eneo muhimu ambapo kila wakati Baraza linapofanya jukumu lake la uwakilishi wakati wa kuwasilisha maoni yake kwa Mdhibiti kuhusu bei za huduma huangaliwa kwa makini sana.

7. Usimamizi Huru wa Huduma

Huduma ya majisafi na uondoaji majitaka mijini itaendeshwa na vyombo vinavyojitegemea na vilivyo karibu na walengwa. Uendelezaji wa huduma hizi utasimamiwa kwa pamoja ili kuhakikisha ufanisi na

uwajibikaji.

8. Ushiriki wa Sekta Binafsi

Sekta Binafsi itawekewa mazingira mazuri ya kuwekeza na kuendesha huduma ya majisafi na uondoaji majitaka mijini. Ushirikiano huu utasaidia kuboresha huduma na kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma hizi.

9. Uboreshaji wa Uhusiano kati ya Sekta ya Umma na Binafsi

Uhusiano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi utaboreshwaa na kuendelezwa kadiri iwezekanavyo. Ushirikiano huu utahakikisha huduma bora na endelevu za majisafi na usafi wa mazingira.

10. Mfumo wa Kisheria wa Usimamizi

Mfumo wa kisheria wa usimamizi utakuwa huru, wa uwazi na wa haki kwa wote. Hii itahakikisha kuwa masuala yote yanayohusu usambazaji wa maji na uondoaji wa majitaka yanashughulikiwa kwa haki na uwazi.

11. Tathmini ya Athari za Mazingira

Tathmini ya athari katika mazingira itakuwa ni ya lazima katika kuandaa miradi mipy ya majisafi na majitaka. Hii ni ili kuepuka athari mbaya za kimazingira na kuhakikisha miradi inatekelezwa kwa njia endelevu.

Misingi hii ni muhimu kwa kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora na endelevu za majisafi na uondoaji majitaka mijini. Kwa mtumiaji, kuelewa misingi hii itaongeza ufahamu wake na kujuu hatua za kuchukua wakati wa kuomba au kutumia huduma za maji nchini. Pia kwa kufuata misingi hii serikali, mamlaka za maji, na wananchi wataweza kushirikiana kwa ufanisi katika kuboresha huduma hizi muhimu kwa maendeleo ya jamii.

“ **Mfumo wa kisheria wa usimamizi** utakuwa huru, wa uwazi na wa haki kwa wote. Hii itahakikisha kuwa masuala yote yanayohusu usambazaji wa maji na uondoaji wa majitaka yanashughulikiwa kwa haki na uwazi.

HabariPicha



Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Mkao wa Kigoma pamoja na wanafunzi wa Klabu ya EWURA CCC, Shule ya Sekondari Rusimbi baada ya Kamati kutembelea shulenii hapa, Juni, 2024 Picha zote na Mpigapicha Wetu



Afisa Msaidizi Huduma kwa Wateja na Utawala Bi. Anadorice Komba akitoa elimu kuhusu kazi za Baraza kwa wananchi wa Mtaa wa Bunukangoma mwezi Mei, 2024. Picha zote na Mpigapicha Wetu




Mjumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma zinazodhibitiwa na EWURA Mkao wa Kilimanjaro Bw. Muhsin Swai (katikati), akieleza wajibu wa kutunza miumbombini ya maji kupitia kipindi cha Radio KR FM iliyoipo mjini Moshi, hivi karibuni.. Picha zote na Mpigapicha Wetu

HabariPicha



Mwenyekiti ya Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Mkoza wa Pwani Bi. Doris Elijah akitoa elimu hivi karibuni kuhusu matumizi sahihi ya huduma za nishati na maji kwa wanafunzi wa Shule Msingi Kibahanamo iliyopo mjini Kibaha.. Picha zote na Mpigapicha Wetu



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Bumai, Bukoba vijijini katika picha ya pamoja na Katibu wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Mkoza wa Kagera ndugu Eustadi Katunzi, baada ya kutoa elimu kwa wanafunzi hao kuhusu kazi za EWURA CCC.. Picha zote na Mpigapicha Wetu



Mjumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Mkoza wa Lindi, ndugu Salumu Dallaly (wa nne kulia) katika picha ya pamoja na watoa huduma za afya ngazi ya jamii baada ya kuwaelimisha kuhusu vidokezo muhimu ya matumizi ya umeme, gesi na maji. Picha zote na Mpigapicha Wetu

Umuhimu wa kuepuka mafundi 'vishoka' wa umeme

Na Wadi Omari, Geita

Ufungaji wa mifumo ya umeme ndani ya majengo ni kazi inayohitaji umakini mkubwa na utaalamu wa hali ya juu. Kutohana na umuhimu huu, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) ilitunga Kanuni Mwaka 2022 ziit-wazo Kanuni za Umeme (Huduma za Ufungaji Wa Mifumo Ya Umeme), 2022, GN. 113 ili kudhibiti kazi za mafundi wa umeme.

Kanuni hizi zinahakikisha kuwa mafundi wanaofanya kazi ya ufungaji wa mifumo ya umeme lazima wawe na leseni kutoka EWURA kama inavyoainishwa kwenye Kanuni ya 4-14 ya Kanuni tajwa.

Aidha, ziko hatari na hasara za kutumia mafundi wasio na leseni kwa mujibu wa Kanuni hizi amba-po mtumiaji wa huduma za umeme anaweza kuathirika nazo. Kwa nini unapaswa kuepuka mafundi wa umeme wasio na ujuzi na wasio na leseni kutoka EWURA ni swali linajibowi na Makala hii:-

1. Usalama wa Watu na Mali

Mafundi wasio na leseni mara nyingi hawana elimu na mafunzo rasmi ya usalama yanayohitaji-

ka kwa ajili ya kufunga mifumo ya umeme. Hii inaweza kusababisha ajali za umeme kama vile hitilafu za umeme ndani ya nyumba/jingo lako mara kwa mara, moto, au milipuko ambayo inaweza kujeruhi watu na kuharibu mali.

4. Kuthibitishwa kwa Vifaa vya Umeme

Mafundi wasio na leseni wanaweza kutumia vifaa visivyo na ubora au vilivyopigwa marufuku, ambavyo vinaweza kusababisha matatizo ya kiufundi na hatari za usalama.

5. Uaminifu na Uadilifu

Mafundi wenye leseni wamepitia mafunzo maalumu na wana uzoefu wa kufanya kazi kwa viwango vya juu vya ubora. Kwa upande mwagine, mafundi wasio na leseni wanaweza kutumia vifaa duni au mbinu zisizofaa, ambazo zinaweza kusababisha mifumo isiyofanya kazi ipasavyo au kushindwa kabisa. Ubora wa kazi huhakikisha ufanisi wa mfumo wa umeme na maisha marefu ya vifaa.

3. Ufutililaji na Udhibiti

EWURA inasimamia na kudhibiti shughuli za mafundi wenye leseni ili kuhakikisha wanazingatia sheria na kanuni za sekta ya umeme. Hii inajumuisha ufutililaji wa huduma zinazotolewa na mafundi hao na kuchukua hatua za kinidhamu pale inapobidi (Kanuni ya 13 (1) (a-e)). Mafundi wasio na leseni hawako chini ya usimamizi wa EWURA, hivyo ni vigumu kuwawajibisha endapo watafanya kazi chini ya viwango.

6. Garama za Ziada

Wakati mfumo wa umeme unafungwa vibaya, unaweza kuhitaji matengenezo ya mara kwa mara na marekebisho, ambayo yanaweza kuongeza garama za muda mrefu. Pia, kutokea kwa ajali au moto kuna weza kusababisha garama kubwa za fidia na matengenezo.

Kwa kuzingatia sababu hizi, ni dhahiri kwamba kutumia mafundi wenye ujuzi na kupewa leseni na EWURA ni chaguo bora kwa usalama, ubora, na thamani ya muda mrefu ya mifumo ya umeme katika jingo lako.



Baadhi ya mafundi umeme kutoka mikoa ya Kanda ya Ziwa wakisikiliza kwa makini maelezo ya kitaalamu kutoka kwa Bw. Shabani Hussein Hegga wa Kampuni ya Umeme, T.L.G, kuhusu namna ya kuchunguza mita za umeme katika majengo makubwa. Zoezi hili liliratibiwa na Ofisi ya EWURA Kanda ya Ziwa na kufayika mijini Geita, hivi karibuni. Picha na Wadi Omari



Uelimishaji

Mjumbe wa Kamati ya Watumiaji wa huduma za Nishati na Maji Mkoa wa Tanga Bi. Bertha Maqway akitoa elimu juu ya Baraza na kazi zake kwa wateja na wafanyabiashara wa soko la Mlango wa Chuma. Picha na Nuru Zuberi

Wananchi masokoni wafikiwa

Na Benjamini Paul, Tanga

Kamati ya Watumiaji ya EWURA CCC mkoani Tanga imeamua kutoka na kuwafuata wananchi katika maeneo mbalimbali wanakofanya shughuli zao ikiwa ni pamoja na kuweka kambi maeneo ya soko la Mlango wa Chuma ili kutoa elimu kuhusu huduma za nishati na maji.

Hatua hiyo ni sehemu ya kazi ili yopangwa na Kamati hiyo kwa lengo la kutoa elimu kuhusu kazi za Baraza kwa wafanyabiashara wa soko hilo pamoja na wateja wanaofika kununua bidhaa sokoni hapo.

Akizungumza katika banda la Baraza, Katibu wa Umoja wa Wafanyabiashara kwenye Soko hilo Bw. Abdallah Ramadhani alilipongeza Baraza kwa kutoka na kukutana na wananchi kwani wengi hawana elimu ya kutosha kuhusu huduma za nishati na maji wanazotumia na kupelekea kupoteza haki zao au kutopata ufumbuzi wa matatizo yao.

"Kwanza niwapongeze kwa ujio wenu kwani kumesaidia kuwapa watu elimu na kujua haki zao. Wengi

wetu hatukuwa na uelewa wa haki zetu kama vile kupewa taarifa kuhusu upatikanaji wa huduma, muda wa siku 30 kulipa bili tangu inapotoka na mengine mengi mliyotufundisha. Kukosa uelewa katika mambo haya yamekuwa yakitusababishia wakati mwingine kukosa haki zetu au kushindwa kupata utatuzi wa changamoto zinazotukibili," alisema Bw. Ramadhan.

Akizungumza baada ya zoezi hilo la uelimishaji Afisa Msaidizi Huduma kwa Wateja na Utawala kutoka EWURA CCC Mkoa wa Tanga Bi. Nuru Zuberi alisema, kufuatia kambi hiyo ya siku mbili Kamati hiyo imefanikiwa kutoa elimu kuhusu Baraza na kazi zake kwa watu wapatao 350. Maeneo mengine ya uelimishaji yamejumuisha haki na wajibu wa mtumiaji pamoja na vidokezo muhimu kuhusu matumizi ya huduma za nishati na maji.

Bi. Zuberi alisema, pamoja na kutoa elimu katika soko hilo, Kamati hiyo ilipokea jumla ya malalamiko 12 kutoka kwa watumiaji wa huduma za nishati na maji na kwa kushirikiana na watoa huduma malalamiko hayo

yalipatiwa ufumbuzi ambapo kati yake 11 yalihusu huduma za maji na 01 ililhusu umeme.

Bi. Nuru Zuberi alisema kuwa Kamati ina jukumu la kuwatetea watumiaji wa huduma za nishati na maji katika kuhakikisha maslahi yao yanalindwa na kwa kutambua kuwa si rahisi watu wote kufika ofisini na kupata elimu ndio maana Kamati hiyo iliona ni vyema kuwafuata watumiaji wa huduma hizo katika maeneo yao ya kazi ili kuwafikishia elimu pamoja na kusikiliza changamoto na malalamiko yanayohusu huduma za nishati na maji.

"Tumeona siyo rahisi watu wote kufika ofisini kwetu kupata huduma na badala yake tukaamua kuwafikia katika maeneo yao ya kazi ili kuwafikishia elimu juu ya huduma umeme, maji, mafuta na gesi pamoja na kupokea malalamiko yao," alisema Bi. Nuru.

Kamati ya Watumiaji ya EWURA CCC Mkoa wa Tanga imekuwa na utaratibu wa kufanya uhamasishaji na uelimishaji katika maeneo mbalimbali yenye mijumuisho wa idadi kubwa ya watu kama masokoni, mikutano ya hadhara ya mitaa, vijiwe vya bodaboda pamoja na uhamasishaji wa mtu mmoja mmoja kama vile nyumba kwa nyumba kwa lengo la kuhakikisha maslahi ya watumiaji wa huduma za nishati na maji yanawakilishwa vyema.

Huu ndio umuhimu wa Mtandao wa Majitaka

Na Chipegawai Samwel, Morogoro

Mamlaka za maji zinalo jukumu kisheria chini ya kifungu namba 13 (1) cha Sheria namba 5 ya Maji ya mwaka 2009 ya kutoa huduma ya majisafi pamoja na usafi wa mazingira.

Mtandao wa majitaka ni mfumo au ni bomba linalopita katika sehemu mbalimbali za mitaa/makazi ya watu kwa ajili ya kukusanya maji yaliyotumika na kuyasafirisha kwenza maeneo maalum yaliyotengwa.

Maji yaliyotumika yanaweza kuwa ni maji toka maliwtoni, maji yaliyotumika kuoshea vyombo, maji yaliyotumika kupigia deki, au kufulia n.k., ambayo si safi na salama. Mamlaka huyakusanya majitaka yote kwa wateja waliojiunga na mtandao wa majitaka na kuyapeleka kwenye maeneo maalumu kwa ajili ya kutibiwa na baadae kuruhusiwa kuingia mtoni.

Kuna faida nyingi za kuijunga na kutumia mfumo wa majitaka (sewage system). Hizi hapa ni faida tano za kutumia mfumo huu:

Usafi na Afya Bora

Mfumo wa majitaka unahakisha kwamba majitaka yanakuanya na kusafirishwa kutoka

majumbani, maeneo ya biashara, na viwanda hadi kwenye mitambo ya kutibu majitaka. Hii inapunguza hatari ya magonjwa yanayosambawza na maji kama kipindupindu na homa ya matumbo, ambayo yanawenza kusambazwa kwa njia ya maji machafu.

Kuhifadhi Mazingira

Mfumo wa majitaka unaopatikana vizuri unapunguza uchafuzi wa mazingira. Majitaka yaliyosafishwa yanaweza kutolewa kwenye mitambo ya kutibu majitaka kwa njia inayofaa kwa mazingira, ambayo inapunguza athari kwa mifumo ya maji ya asili kama mito, maziwa na bahari.

Ufanisi wa Rasilimali

Kutumia mfumo wa majitaka husaidia katika matumizi bora ya rasilimali maji. Badala ya kutumia majisafi kwa kazi za kutolea taka, mfumo wa majitaka unawezesha maji kurejeshwa kwa matumizi mengine baada ya kutibiwa ipasavyo.

Ukamiliu wa Miundombinu ya Mji

Mifumo ya majitaka husaidia katika maendeleo ya miundombinu ya miji kwa kusambaza huduma

bora za usafi wa mazingira. Hii ni muhimu sana katika maeneo ya mijini ambapo idadi ya watu inazidi kuongezeka, na mahitaji ya usafi na mazingira safi yanakuwa muhimu zaidi.

Kukuza Uchumi

Uwekezaji katika miundombinu ya majitaka huchangia ukuaji wa uchumi kwa kuboresha mazingira ya biashara na kuongeza ufansi wa huduma za mijini. Kwa mfano, miji ambayo ina mifumo ya majitaka iliyoundwa vizuri inakuwa na rasilimali bora za mazingira amba zo zinavutia uwekezaji na kukuza biashara.

Matumizi sahihi ya mtandao wa majitaka ni kama ifuatavyo:-

- Epuka kutiririsha maji ya mvua kwenye mtandao wa majitaka
- Epuka kutupa taka ngumu kwenye mtandao wa maji taka kama vile makopo, nguo, tauko za kike, na hata pampas za watoto
- Weka/jenga chekeche juu ya chemba za majitaka ili kuzuia taka ngumu kuingia katika mtandao wa majitaka

Watumiaji tuna wajibu wa kuitunza miundombinu ya majitaka, kutoa taarifa haraka juu ya uvujaji wa mtandao wa majitaka, kufichua wahujumu miundombinu ya majitaka na wanaotupa taka ngumu na kulipa bili za majitaka pindi zinapotoka ili kuepuka kusitishiwa huduma hizo.



MANAWASA

EPUKA BILI KUBWA KWA KUFANYA YAFUATAYO

1. Epuka kumwaga maji yanayoweza kutumika kwa matumizi mengine.
2. Weka utaratibu wa mara kwa mara wa kuchunguza miundombinu ya maji yako ili kutambua mivujo.
3. Jivekee utaratibu wa kuhifadhi maji kwenye madumu au tanki na tumia kwa uangalifu.
4. Hakikisha unafunga vizuri koki za bomba la maji mara baadaye matumizi.

**WASILIANA NASI
HUDUMA KWA WATEJA**

+255 684 562 464 || +255 788 446 561

 ManawasaTz



Ndugu Mtejal!

Sasa unaweza kutoa tarifs ya hitlifu ya umeme katika eneo lako **ndani ya Mkoa wa Manyara**

kwa kutupigia katika nambari za simu zifurato

**0748 550 000
0689 795 599**

Au kwa kutembelea ofisi zetu za **TANESCO** zillizopo jirani nawe.

#TupoKazini

Mambo muhimu kuepuka ajali zitokanazo na umeme

Na Geofrey Sokesia, Singida

Ifahamike kuwa umeme ni huduma muhimu sana katika maisha ya binadamu na suala zima la uchumi. Mafanikio makubwa ya kiuchumi duniani yamekuwa yakichagizwa na uwepo wa umeme kwa katumika katika shughuli za viwandani, kwenye taasisi za utoaji huduma kama vile mahospitalini, taasisi za kidini, pamoja na taasisi za elimu.

Pamoja na faida kubwa ya huduma ya umeme, endapo utatatumika vibaya au pasipo tahadhari unaweza kusababisha majanga ya moto na kusababisha watu kupoteza Maisha na mali zao ikiwa ni pamoja na kukwamisha shughuli za kiuchumi.

Mbali na majanga ya moto, umeme pia kama utatumiaka bila kufuata mashariti huweza kusababisha maafa hata kwa viumbe wengine au kuharibu mitambo ambayo huendeshwa kwa kwa kutumia nishati hiyo.

Itakumbukwa mwaka 2021 tarehe 16 Novemba kulitokea ajali ya moto katika soko la Manzese katika Halmashauri ya Mji wa Tunduma na kuteketeza maduka 46 katika soko hilo na hivyo kupelekea hasara kubwa kwa wafanyabiashara wa soko hilo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyowekwa kwenye tovuti ya Halmashauri hiyo (<https://tundumac.go.tz/new/hitilafu-ya-umeme-chanzo-cha-ajali-ya-moto-soko-la-manzese-rc-mgumba-ameiagiza-tanesco-kupitia-mfumowa-masoko-yot>) mnamo tarehe 27 Novemba, 2021 inaonesha kuwa baada ya uchunguzi kufanya ilibainika kuwa chanzo cha ajali hiyo ilikuwa ni hitilafu ya umeme ambayo ilisababisha na watumiaji wa huduma hiyo kutofuata taratibu na mashari ya matumizi ya umeme yaliyowekwa na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).

Kwa mujibu wa taarifa hiyo miongoni mwa wafanyabishara waliounganishwa na huduma ya umeme na TANESCO walikiuka mkataba kama vile kuijunganishia umeme kiholela. Katika taarifa hiyo inaonesha kuwa ni wateja 13 tu ndio walikuwa na mkataba na wengine walijunganishia kiholela na hivyo kusababisha ajali hiyo.

Hivyo basi makala hi inalenga kutoa elimu kuhusu mambo ya kuzingatia ili kujiepusha na athari zinazoweza kusababishwa na matumizi mabaya ya umeme:-

i. Inashauriwa na kukatazwa kujenga nyumba, kufanya biashara, shughuli za kilimo na hata shughuli zozote zingine za kiuchumi au kijamii chini ya nyaya za umeme.

ii. Wananchi wanatakiwa kuwa makini wakati wa usimikaji antena za televisheni kwani mara nyingi kumekuwa na ajali za namna hii pale mtu anapokuwa anajaribu kusimika antena na ule mti au bomba lenye antena likagusa nyaya za umeme ambapo hali hiyo huweza kuleta ajali na pengine kusababisha vifo.

iii. Inapoteka changamoto ya umeme ndani ya nyumba yako ni vyema kutumia mafundi wenye leseni kutoka EWURA kwa kuwa kutumia mafundi wasio na elimu ya kutosha juu ya umeme huweza kuleta ajali za moto na maafa.



Wananchi wakifanya shughuli za biashara chini ya miundombinu ya umeme. Jambo hili ni hatari kwa usalama wa afya na mali zao.

Picha kwa hisani ya ukurasa wa facebook wa TANESCO

iv. Kukaa mbali na miundombinu ya umeme hasa nyakati za mvua na upopo mkali, kwani wakati wa mvua na upopo miundombinu ya umeme inaweza kudondoka na kuleta hatari kwa watu walipo meneo hayo, pia inakatazwa watu kujificha chini ya transfoma za umeme wakati wa mvua au kufanya biashara chini ya transfoma.

v. Wazazi tuwakataze watoto kubembea au kuchezea nyaya zinazoshikilia nguzo maarufu kama "stay wires." Nyaya hizi zinaweza kuwa na umeme, na hivyo kusababisha maafa kwa yeote atakayezishika. Hii pia inasitisizwa kwa watu wote kutoleshika nyaya za umeme zilizoanguka chini kwani zinaweza kuwa na umeme na pengine kuleta maafa.

vi. Ni hatari kubeba vitu vyenye kimo kirefu wakati wa kupita chini ya nyaya za umeme. Kufanya hivyo huhatarisha maisha kwa anayefanya hivyo pamoja na kuhatarisha maisha ya watu wengine walio karibu pamoja na mali zao. Pia kwa madereva wa magari makubwa ya kubeba mizigo mikubwa au mirefu wachukue tahadhri wakati wa kupita chini ya mifumo ya umeme kwani inaweza kuhatarisha maisha yao na miundombinu ya umeme.

vii. Wazazi tuwazuie watoto kuchenza karibu na miundombinu ya umeme au kuacha tabia ya kulenga mawe nyaya au vikombe vya umeme kwani kufanya hivyo huweza kusababisha moto na hatari kwa maisha ya watu na uharibifu wa miundombinu.

viii. Kujiepusha na tabia ya kuwashaa moto chini ya miundombinu ya umeme. Wako baadhi ya watu wanaofanya shughuli za kilimo kuwashaa moto chini ya miundombinu ya umeme na hivyo kupelekea kuungua kwa nguzo za umeme ambapo kupelekea nguzo kuan-guka na kuleta hatari zaidi na kuathiri miundombinu ya umeme na maisha ya watu.

Wananchi tunatakiwa kuchukua tahadhari kwa kuepuka kufanya mambo ambayo yameelezwa hapo juu na kutoa ushirikiano kwa TANESCO katika kulin-dha miundombinu. Ifahamike kuwa TANESCO ni mali ya umma hivyo sote tunao wajibu wa kulinda miundombinu ya umeme na kuchukua tahadhari ya hatari zitokanazo na umeme.

Tahadhari

IRUWASA yapongezwa, matumizi ya mita za malipo ya kabla

Na Brenda Magoma, Iringa

Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) limeipongeza Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Iringa (IRUWASA) kuwa Mamlaka ya kwanza kutumia mita za malipo ya kabla.

Pongezi hizo zimetolewa hivi karibuni na Katibu Mtendaji wa Baraza Bi. Stella Lupimo wakati wa ziara ya kutembelea Mamlaka hiyo ambayo ilijumuisha Wajumbe wa Baraza, Sekretarieti na Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Mkoa wa Iringa.

Bi. Lupimo alisema kuwa suala la wateja kuwa na mita za malipo ya

“Moja ya shughuli za Baraza ni kuzishauri mamlaka za maji nchini ambapo moja ya eneo ambalo Baraza kwa muda mrefu sasa limekuwa likisisitiza ni umuhimu wa mamlaka za maji kuwafungia wateja wake mita za malipo ya kabla (pre paid meters) kwani tunaamini kuwa hii ni njia pekee ya kupunguza malalamiko kutoka kwa watumiaji kuhusu bili za kubambikizwa, hivyo tunapongeza IRUWASA kwa kuongoza katika eneo hilo,” alisema Bi. Lupimo.

kabla litawapunguzia malalamiko hasa yanayohusu bili kubwa.

“Moja ya shughuli za Baraza ni kuzishauri mamlaka za maji nchini ambapo moja ya eneo ambalo Baraza kwa muda mrefu sasa limekuwa likisisitiza ni umuhimu wa mamlaka za maji kuwafungia wateja wake mita za malipo ya kabla (pre paid meters) kwani tunaamini kuwa hii ni njia pekee ya kupunguza malalamiko kutoka kwa watumiaji kuhusu bili za kubambikizwa, hivyo tunapongeza IRUWASA kwa kuongoza katika eneo hilo,” alisema Bi. Lupimo.

Aliongeza kuwa, Baraza kwa muda mrefu limekuwa na matamano makubwa ya kuja IRUWASA kuona utendaji kazi wao hususani



Mkurugenzi wa Usambazaji Maji na Usimamizi wa Mazingira wa IRUWASA Mha. Fabian Maganga (wa kwaza kulia) akionesha mita za maji za malipo ya kabla kwa ujumbe wa Baraza uliotembelea Mamlaka hiyo hivi karibuni. Picha na Brenda Magoma



Mha. Fabian Maganga akitoa maeleo kwa Ujumbe wa Baraza kuhusu namna Mamlaka ya IRUWASA inavyotibu maji katika eneo la Ndiuka, Mkoa wa Iringa. Picha na Brenda Magoma

kwenye matumizi ya mita za malipo ya kabla lakini pia walitamani kufahamu IRUWASA imewezaje na inatatuaje changamoto za wateja wanaotumia mita hizo ili kuongeza ufahamu utakaosaidia katika jukumu na takwa la kisheria la kushauri.

Naye Mkurugenzi wa Usambazaji Maji na Usimamizi wa Mazingira wa IRUWASA Mhandisi Fabian Maganga alisema kuwa kabla ya uwepo wa mita za malipo ya kabla IRUWASA ilikuwa ikipokea malalamiko mengi ya kuwepo kwa bili kubwa, na bili za kukadiria lakini baada ya mita za malipo ya kabla kufungwa kwa wateja malalamiko yamepungua kwa asilimia kubwa na pia makusanyo ya mamalaka yameongezeka.

"Awali tulikuwa na changamoto ya kupokea malalamiko mengi kutoka kwa wateja kuhusu ankara kubwa na bili za kubambikizwa, lakini kwa sasa Mamlaka inatumia refa (mita za malipo kabla) halali am-baye haipendelei mtu. Tunaona matumizi ya mita za malipo ya kabla ni

“
Mimi niwapongeze sana IRUWASA kwa hatua hii na uthubutu mliouonesha wa kuwafungia mita za malipo ya kabla wateja wengi. Hakika itawapunguzia changamoto ya makusanyo ya mapato kwa kudhibiti madeni...

suluhisho kubwa katika malalamiko ya bili bambikizi na pia inampa nafasi mteja kununua maji kulingana na uwezo wake kwa wakati huoi," alisema Mhandisi Maganga.

Alisema uwepo wa mita za malipo ya kabla umewarahisishia kazi ya kukusanya mapato ambapo asilimia

96 ya mapato yanatokana na matumizi ya mita za malipo ya kabla. Pia Mamlaka imekufunga mita hizo kwa wateja zaidi ya 6000 na miongoni mwa wateja hao ni taasisi za umma, na wateja wa kawaida.

Naye Mjumbe wa Baraza Baraza Bi. Hawa Ng'humbi aliwapongeza IRUWASA kwa hatua ya uthubutu wa kuwafungia wateja wao mita hizo kwa sababu zinasaidia kupunguza changamoto na pia kujua matumizi yao halali.

"Mimi niwapongeze sana IRUWASA kwa hatua hii na uthubutu mliouonesha wa kuwafungia mita za malipo ya kabla wateja wengi. Hakika itawapunguzia changamoto ya makusanyo ya mapato kwa kudhibiti madeni na pia watumiaji watajua kiwango sahihi cha matumizi yao," alisema Bi. Ng'humbi.

Mwisho, Bi. Ng'humbi aliuomba uongozi wa IRUWASA kuendeleza ushirikiano kati yake na Baraza kwa maslahi mapana ya watumiaji wa huduma zinazotolewa na mamlaka hiyo.

Toeni elimu kwa wateja wenu matumizi ya gesi - RCC Singida

Na Theresia Mande, Singida

Mawakala wa uuzaaji wa gesi za kupikia za Oryx mkoani Singida wameaswa kuwapatia elimu wateja wao juu ya matumizi sahihi na hatari ambazo zinaweza sababishwa na matumizi mabaya ya gesi.

Hayo yamesemwa hivi karibuni na Bi. Evarista Lucas ambaye ni Mjumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Mkoa wa Singida wakati akiongea na mawakala wa uuzaaji wa gesi ya Oryx Manispaa ya Singida.

Bi. Lucas aliyasema hayo kupitia mukutano wa mwaka ulioandaliwa na kampuni hiyo ya uuzaaji gesi za kupikia uliofanyika mjini Singida ukiwa na lengo la kuwapatia elimu wauzaaji wa gesi hiyo.

Bi. Lucas aliwahimiza mawakala hao kuhakikisha wanatimiza

matakwa ya kisheria na wajibu wa kazi yao ikiwemo kuwapa elimu wateja wao kuhusu masuala ya usalama na afya za watu pamoja na mali zao wakati wanapotumia nshati ya gesi.

Evarista aliwaomba mawakala hao kuwafundisha wateja wao namna ya kuunganisha mitungi ya gesi na majiko hasa kwa wateja wanaonunua vifaa hivyo kwa mara ya kwanza ili kuepuka madhara yanayoweza kutokea kutokana na uvujaji wa gesi inapokuwa imeunganishwa vibaya.

"Usione aibu kumuuliza mteja wako endapo ni mara yake ya kwanza kutumia gesi, kisha muelekeze kwa vitendo namna ya kuunganisha na kuwashaa jiko," alielea Bi. Lucas

Aidha, Bi. Lucas aliwasisitiza mawakala hao kuwaelimisha wateja wao juu ya umuhimu wa kupima uzito wa mitungi ya gesi wakati wa kununua ili kuhakiki uzito ulioand-

ikwa kwenye mtungi na ule ambaa unaonekana kwenye mzani kama vinashabihiana.

Aliwaomba mawakala hao kuwapa elimu wateja wao juu ya matumizi sahihi ya gesi pamoja hatari zake, huku akitaja baadhi ya mambo ambayo mtumiaji anatakiwa kuelimishwa kabla ya kuanza kutumia nishati ya gesi ikiwemo kukagua na kujiridhisha lakiri ya mtungi anaonunua kuwa ni ya kampuni husika, kupima uzito wa mitungi ili kujiridhisha na uzito wa gesi anayonunua, kusafirisha mitungi ya gesi ikiwa imesimamishwa wima, kuhi-fadhi mitungi sehemu yenye hewa ya kutosha na mbali na vyanzo nya moto.

"Nawaomba mzingatie kufanya yale yanayotakiwa ikiwemo kuuza mitungi yenye lakiri na sio kuuza mitungi bandia, kupima uzito wa mitungi kwa wateja wakati wa mauzo na kuwelimisha juu usafirishaji



UTAFITI WA UPIMAJI WA HUDUMA ZA TANESCO



Kuanzia Tarehe
11 - 28 Mei 2024

Kuwa huru tupatie
maoni yako na tushauri



SCAN
KUTUPIMA...



#TupoKazini

salama wa mitungi ili kujiepusha na hatari kwa wateja wenu, lakini pia uzeni gesi kwa kufuata bei elekezi, alisema Bi. Lucas"

Aidha aliwahimiza wafanya-biashara hao hususani wale waagizaji wa jumla na wasambazaji wakubwa (LPG Super Dealers) kuhakikisha kuwa wana leseni ya EWURA.

Kwa upande wake Meneja Wakala wa Vipimo (WMA) Mkoa wa Singida ndugu Willy Amosi aliwataka mawakala hao kuhakikisha wanaweka na kutumia mizani za kisasa katika maduka yao ili kuhakikisha wateja wao wanapata bidhaa hiyo kwa kipimo sahihi kinachoakisi ghamra halisi ya bidhaa hiyo.

"Nipende kuwaasa kuwa ni lazima kwa kila wakala au muuzaji wa mitungi ya gesi kuwa na mzani wa kidigitali ambao atautumia kumpimia mteja mtungi wa gesi kabla hajamuuzia. Hii inahakikisha kuwa mtumiaji anapata bidhaa kamili inayolingana na thamani ya pesa anayolipa," alisema Bw. Amosi.

Aidha katika suala la usalama kwa wauzaji na watumiaji wa gesi,

“
Nipende kuwaasa
kuwa ni lazima kwa kila wakala au muuzaji wa mitungi ya gesi kuwa na mzani wa kidigitali ambao atautumia kumpimia mteja mtungi wa gesi kabla hajamuuzia. Hii inahakikisha kuwa mtumiaji anapata bidhaa kamili inayolingana na thamani ya pesa anayolipa.

Afisa kutoka kitengo cha habari Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Konstebo Rahma Athumanli aliwahimiza mawakala hao kuwa na vifaa nya kuzimia moto katika ofisi zao.

"Kama tunavyojuu gesi hii tunayoiuza ni matokeo ya uchakataji

mafuta petroli kwa hiyo isipotumi-ka au kuhifadhiwa vizuri inaweza kulipuka na kusababisha madhara, hivyo ni vema kuchukua tahadhari kwa kuwa na vifaa nya kuzimia moto kwani huwezi kujua ni wakati gani janga linaweza kutokea," alieleza Konstebo Rahma.


"Ni muhimu kuwa na vifaa nya kuzimia moto kwenye nyumba zetu ili kujihami wakati wa hatari. Viko vifaa pia nya kung'amua moshi ambavyo vitatoa tahadhari endapo kuna harufu ya moshi itaanza kutokea," alisema Konstebo Rahma.

Kwa upande mwengine wakala hao waliupongeza uongozi wa EWURA CCC, Oryx, Jeshi la Zimamoto pamoja na ofisi ya Wakala wa Vipimo mkoani Singida kwa kuwapatia elimu juu ya namna sahihi ya kufan-ya biashara hiyo.

Akiongea kwa niaba ya mawaka-la wenzake wa uuzaaji wa gesi Bi. Salma Athumanli alisema "kupitia mukutano huu tumepata maarifa ma-pya ambayo yataenda kutusaidia katika biashara zetu, hivyo tunaahidi kwenda kuwapatia elimu hii wateja wetu pia."

Uelimishaji

MAMLAKA YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA TABORA (TUWASA)



UFAHAMU MKATABA WA HUDUMA KWA MTEJA

HAKI ZA MTEJA

- **Kupata huduma bora**
- **Kupata taarifa sahihi na kwa wakati**
- **Kutoa, kuwasilisha maoni, pongezi au malalamiko**
- **Kupewa faragha na kutunziwa siri kuhusu huduma iliyotolewa**
- **Kupata huduma bila kubaguliwa**

ba taarifa imayohusu
huduma ya maji.



0800780063



Watumiaji wakubwa wa nishati safi wafikiwa

Na Lusekelo Kajela, Mbeya

Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) limeongeza juhudzi zake katika kutoa elimu kuhusu matumizi sahihi na salama ya nishati safi ya kupikia na hivi karibuni limeanza kuwafikia watumiaji wakubwa wa huduma hizo katika taasisi mbalimbali za serikali na zisizo za serikali.

Watumiaji wakubwa wa gesi, wanaojulikana kama "bulk consumers," ni wale wenye matumizi makubwa ya nishati ya gesi na ambao wanafungiwa matanki makubwa ya gesi nje ya majengo yao. Matanki haya hujazwa gesi kwa kutumia magari maalum na gesi hiyo husafirishwa kupitia mfumo wa mabomba na valves hadi jikoni.

Matumizi ya gesi yanazo faida nyingi kwa watumiaji kama itakavyoleezwa katika Makala hii. Kutokana na faida hizo, EWURA CCC inaunga mkono jitihada za Serikali katika kampeni yake ya matumizi ya nishati safi ya

kupikia, kama inavyotiliwa mka zo na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Ifahamike kwamba, kupitia Mkakati wa Nishati Safi nchini, Tanzania inalenga kufikia asilimia 80 ya Watanzania wanaotumia nishati safi ya kupikia nchini, ifikapo mwaka 2034.

Ili kufikia malengo hayo na kuunga mkono juhudi hizo za Serikali, EWURA CCC imejipambanua wazi kwa kutoa elimu kwa watumiaji wa huduma hizo na kuhamasisha umma wa watanzania wengi zaidi kuhamia katika matumizi sahihi na salama ya nishati safi ya kupikia.

Hivi karibuni EWURA CCC mkoa wa Mbeya ilitoa elimu kuhusu matumizi salama ya nishati safi ya kupikia kwa taasisi mbalimbali ambazo ni watumiaji wakubwa wa nishati safi ya kupikia ikiwemo Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) kikosi cha 44KJ, Chuo cha VETA, na Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Idiga.

Taasisi hizo tayari zinanufaika

Picha ya pamoja ya Wajumbe wa Kamati ya Watumiaji ya Baraza mkoani Mbeya, pamoja na baadhi ya wafanyakazi wa Kampuni ya Taifa Gesi baada ya mafunzo ya matumizi sahihi ya gesi kwa watumiaji wakubwa yaliyotolewa kwa JWTZ, kikosi namba 44KJ Mbalizi, Mbeya.
Picha na Mpigapicha Wetu

na matumizi ya nishati safi na zinapata faida kadhaa muhimu ambazo wewe msomaji wa makala hii tunaamini ungependa kuzifahamu:-

Kuokoa Muda wa Kupika

Gesi ya LPG huivisha chakula haraka na kwa ubora, hivyo kuokoa muda wa kupika. Hii ni muhimu kwa taasisi kama vile shule, hospitali, na mahoteli ambapo muda ni rasilimali muhimu.

Usalama na Urahisi wa Matumizi

Matumizi ya gesi ya LPG ni salama na rahisi. Watumiaji wakubwa hufungiwa vifaa maalum kama vile "Rochester gauge" ambavyo husaidia kupima kiasi cha gesi kilichopopo ndani ya tanki. Hii husaidia kuhakikisha kuwa gesi haiishi ghafla, na inaruhusu kupanga upya namna ya kupata nyingine kabla ya gesi kuisha.

Gharama Nafuu kwa Muda Mrefu

Ingawa gharama za awali za kufunga mfumo wa gesi ya LPG zinaweza kuwa kubwa, matumizi ya muda mrefu yanawenza kuwa na gharama nafuu ukilinganisha na kuni au mkaa. Hii ni kwa sababu gesi ina nguvu zaidi na huchukua muda mfupi kupika, hivyo kupunguza matumizi ya nishati kwa ujumla.

Utunzaji wa Mazingira

Matumizi ya gesi ya LPG yanapunguza uharibifu wa mazingira unaosababishwa na matumizi ya kuni na mkaa.

Gesi ya LPG haitoi hewa chafu kama vile kaboni nydingi na masizi ambayo huchafua mazingira na kuchangia mabadiliko ya tabianchi.

Afya Bora

Gesi ya LPG haitoi moshi mwiningi kama kuni na mkaa, hivyo kupunguza hatari za kiafya kama vile magonjwa ya kupumua na kansa. Hii ni muhimu sana kwa afya ya wapishi na watu wanakaa karibu na majiko.

Usafi wa Jiko na Vyombo

Gesi ya LPG hutoa joto safi ambalo haliachi masizi kwenye vyombo vya kupikia na kuta za jiko. Hii husaidia kuweka mazingira ya jikoni safi na salama.

Kuaminika kwa Usambazaji

Watumiaji wakubwa wa gesi ya LPG hujaziwa gesi kwa kutumia magari maalum, ambayo huhanikisha kuwa gesi inapatikana kwa wakati na kwa urahisi. Mfumo wa usambazaji wa gesi

kupitia mabomba na "valves" ni wa kuaminika na unafaa kwa matumizi ya kila siku.

Matumizi Mbalimbali

Gesi ya LPG inaweza kutumika katika matumizi mengine kama vile kuendeshea injini na jenreta, hivyo kuongeza ufanisi wa nishati katika taasisi na viwanda.

Kwa ujumla, matumizi ya gesi ya LPG kwa watumiaji wakubwa yanachangia katika maendeleo endelevu, utunzaji wa mazingira, na kuboresha maisha ya watanzania.

Pamoja na faida hizo, zifuatazo ni dondo chache muhimu za kiusalama za kuzingatia wakati wa kutumia nishati ya gesi:

Ukaguzi wa Mabomba na Valves

Fanya ukaguzi wa mara kwa mara wa mabomba na "valves" za gesi ili kuhakikisha hakuna uvujaji.

Kuzima Gesi Baada ya Matumizi

Zima gesi kwenye "valve" kuu baada ya matumizi ili kuzuia uvujaji wa gesi.

Vifaa vya Kuzima Moto

Hakikisha una vifaa vya kuzima moto kama vile kizima moto na blanketi la moto jikoni kwa dharura.

Tahadhabri na Moto

Epuka kutumia gesi karibu na vitu vinavyoweza kuwaka moto kwa urahisi kama vile vitambaa na karatasi.

Kuhifadhi Mitungi ya Gesi

Hifadhi mitungi ya gesi katika sehemu iliyio na uingizaji hewa wa kutosha, mbali na juu na joto kali.

Kupima Uvujaji

Tumia maji na sabuni kupima uvujaji wa gesi kwa kupaka kwenye viunganishi vya mabomba na kuangalia kama kuna mahali panavuja.

Matumizi Salama ya Mitungi

Hakikisha mitungi ya gesi inakaa wima wakati wote wa usafirishaji na usibebi au kuhifadhi mitungi hiyo ukiwa umeinua upande mmoja.

Jedwali kuonesha mahitaji ya gesi kulingana na idadi ya watumiaji

Na	IDADI YA WATU	AINA YA TANKI (DUMPING CYLINDER)
1.	65-250	200kg
2.	251-450	500kg
3.	451-650	1000kg(tani1)
4	651>	Tani1>

Chanzo: Taifa Gas



**TAFADHALI
EPUKA**

- kuunganisha misereji ya mvua katika mtandao wa majitaka
- kuharibu miundombinu ya majitaka
- kutupa taka ngumu katika mtandao wa majitaka.

Kifungu Na.61 cha sheria ya maji Na. 5/2019; kinaainisha kuwa ni kosa kisheria kuharibu miundombinu ya majisafi na majitaka au mali za Mamlaka ambapo adhabu yake ni faini ya kuanzia Tsh.500,000 hadi Milioni 50 au kifungo cha miaka 2 hadi miaka 5.

 @moruwasa  @moruwasa2  0736 737 736  0800751011 (BURE)
www.moruwasa.go.tz

Walalamikia utaratibu mpya wa kuripoti malalamiko ya umeme

Na Geofrey Sokesia, Singida

Wamiliki wa viwanda vya mafuta ya alizeti mkoani Singida wameonesha kutoridhiswa kwao na utaratibu wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) wa malalamiko ya dharura ya umeme kuripotiwa kwenye kituo cha miito ya simu cha makao makuu na baadaye taarifa hiyo kurejeshwa kwenye ofisi za mikoa jambo linalosababisha ucheleweshaji wa utatuza wa malamiko yao.

Haya yameibuka baada ya Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji mkoani Singida kuwatembelea watumiaji wakubwa wa huduma za nishati na maji zinazodhibitiwa na EWURA.

Bwana Khalid Ally ambaye ni Mkurugenzi wa kiwanda cha Mafuta ya alizeti cha Singida Fresh Oil Mill alisema kuwa utaratibu wa malalamiko kupelekwa kwanza makao makuu ya TANESCO unawatia hasara katika biashara zao.

Bw. Ally alisema yeye ni moja ya watumiaji wakubwa wa huduma ya umeme mkoani Singida lakini kwa siku za hivi karibuni amekuwa haridhishwi na utaratibu ambao TANESCO wameuweka wa upokeaji wa taarifa za dharura.

“Mara nyingi nilipokuwa nikipata changamoto ya huduma ya umeme nimekuwa nikijaribu kuwapigia watu wa TANESCO mkoaa wa Singida lakini nimekuwa nikipewa namba ya makao makuu kwanza, na ukipiga namba hiyo ya makao makuu wao

baadaye hurudisha lalamiko hilo kwenye ofisi ya mkoa kwa ajili ya kushughulikiwa,” alisema Bw. Ally

Aliendelea kusema “Hebu fikiria kwa mfano nyumba inauungua moto, unapiga simu makao makuu ndipo wao watoe taarifa kwenye ofisi ya karibu, nadhani mpaka wafike nyumba hiyo itakuwa imeteketea yote. Mimi nashauri TANESCO warudishe simu za dharura kwenye kila ofisi badala ya maalamiko yote ya dharua kuuanza kushughulikiwa makao makuu,”

Naye Bw. Mohamed Khalfan ambaye ni mmliki wa kiwanda cha uzalishaji mafuta ya alizeti kilichopo eneo la Sido Singida, alisema kuwa utaratibu mpya uliowekwa na TANESCO wa simu zote za malalamiko kupokelewa kwanza makao makuu umekuwa ukizorotesha uzalishaji katika kiwanda chake kwani mara nyingi anapopata changamoto ya dharura juu ya huduma ya umeme imekuwa ikichukua karibu siku nzi-ma mpaka wataalamu kufika na kutatta tatizo hiyo.



Meneja wa TANESCO Mkoa wa Singida Mha. Mwamvita Ally akisisitiza jambo wakati wa kikao na Wajumbe wa Kamati ya Baraza ya watumiaji Mkoa wa Singida (hawaonekani katika picha) walipotembelea ofisini kwake, hivi karibuni. Picha na Theresia Mande

“

TANESCO mkoa wa Singida ina namba mbili, moja kwa ajili ya huduma kwa wateja ambayo hushughulikia malalamiko na taarifa zisizo za dharura na nydingine ni kwa ajili ya taarifa na malalamiko ambayo ni ya dharura, namba inayokuwa hewani muda wote.

Khalfan amesema “unapiga simu makao makuu, inachukua muda mpaka upate mhudumu wa kukusikiliza. Baada ya hapo una-subiri taarifa hiyo itumwe kwenye ofisi ya TANESCO iliyo karibu ndipo baadae wataalamu waje, ambapo kwa kipindi chote hicho cha kusubiri shughuli za uzalishaji zinakuwa zimesimama kiwandani.”

Akitolea maelezo hoja hiyo Meneja wa TANESCO Mkoa wa Singida Mhandisi Mwamvita Ally alisema kuwa tayari ofisi TANESCO imekuwa ikipata malalamiko kutoka kwa wateja wao juu ya utaratibu wa simu za taarifa na malalamiko ya dharura kuelekezwa makao makuu.

Mha. Ally alisema “Wateja wamekuwa wakipata changamoto kubwa kwani wamekuwa wakilazimika kupiga simu kwenye kituo cha huduma kwa wateja makao makuu, na wakati mwininge simu zao kusubirishwa au malalamiko yao kutofanikiwa na hivyo kushindwa kutatuliwa kwa wakati.”

Mha. Mwamvita alisema kuwa

kwa sasa Shirika limerudisha huduma ya simu za taarifa na malalamiko katika ngazi za mikoa baada ya kuona kuwa wateja wao wamekuwa wakipata changamoto ya malalamiko yao kushughulikiwa kwa wakati.

“Kwa sasa TANESCO ofisi ya Mkoa wa Singida kitengo cha huduma kwa wateja kinapokea taarifa za

malalamiko ya dharura katika ofisi ya mkoa, hivyo wateja wakipata changamoto wanaweza kupiga simu moja kwa moja ofisi ya Singida na changamoto zao zikatuliwa mara moja bila ucheleweshaji.”

Alieleza kuwa TANESCO mkoa wa Singida ina namba mbili, moja kwa ajili ya huduma kwa wateja ambayo hushughulikia malalamiko na taarifa zisizo za dharura na nydingine ni kwa ajili ya taarifa na malalamiko ambayo ni ya dharura, namba inayokuwa hewani muda wote,” alieleza Mhandisi Ally.

Aliongeza kuwa kwa siku za mbele ni Shirika lina mpango wa kupanua wigo kwa kuanzisha vituo vya kupokea simu na kuhudumia wateja kwenye ofisi zake za wilaya hususan wilaya zile zenye wateja wengi.

Aliwaomba wateja wao kuen-delea kufurahia huduma zao kwani Shirika linaendelea kuboresha huduma zake ikiwemo kutatua malalamiko wateja ndani ya muda mfupi.



ELIMIKA NA TANESCO

Kitaalam inashauriwa kufanya mapitio ya mtandao wa umeme (wiring) ndani ya nyumba kila baada ya miaka mitano kwa kutumia Mkandarasi wa umeme aliye sajiliwa.

Sababu zifuatazo husababisha matumizi yasiyotarajiwa ya umeme ndani ya nyumba:

- 1 **Kuvuja** kwenye maungio dhaifu
- 2 **Kulegea** kwa **maungio** ya nyaya za umeme
- 3 Kutumia waya **mdogo** kuliko mahitaji hivyo kusababisha kupata **joto** na kuongeza **ukinzani** kwenye waya

HabariPicha



Mwenyekiti wa Kamati ya Watumaji wa Huduma za Nishati na Maji mkoani Kigoma, Bi. Rose Kanango (aliyesimama kulia) akifundisha kuhusu vidokezo muhimu vya matumizi ya nishati na maji katika kijiwe cha kahawa, Mtaa wa Bushabani, Kata ya Kibirizi, mjini Kigoma mwezi Juni 2024. Picha zote na Mpigapicha Wetu



Afisa Msaidizi Huduma kwa Wateja na Utawala wa Baraza mkoani Mara Bw. Dennis Ndanu la EWURA CCC eneo la Kivuko cha Mwigobero Kinest, mjini Musoma. Baraza liliweka banda katika eneo hili mapema Juni, 2024 ili kutoka elimu kuhusu masuala muhimu yahusuyo huduma za nishati na maji kwa watu waliopita katika Kivuko hicho. Picha zote na Mpigapicha Wetu



Afisa Msaidizi Huduma kwa Wateja na Utawala wa Baraza mkoani, Iringa Bi. Brenda Magoma (kulia) akitoa akifundisha kuhusu haki na wajibu wa mtumiaji kwa wadau walioshiriki katika mkutano wa wafanyabiashara, Kilolo mjini Iringa, mwezi Juni, 2024. Picha na Painetho Madembwe

HabariPicha



Mwenyekiti wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji mkoa wa Tanga, Bw. Twali Mshare akitoa elimu kwa wanafunzi wa Chuo cha VETA mkoani Tanga kuhusu utaratibu wa kulalamikia huduma za nishati na maji zisizoridhisha ili kupata utatuzi wake, badala ya kunung'unika tu. Picha zote na Mpigapicha Wetu



Mwenyekiti wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji mkoa wa Arusha Mha. Raymond David akitoa elimu kuhusu utunzaji wa miundombinu ya maji na umeme kwa waumini wa Kanisa la KKKT Usharika wa Engarenaro jijini Arusha, mwezi Mei, 2024.. Picha zote na Mpigapicha Wetu



Mwenyekiti wa Kamati wa Huduma za Nishati na Maji Mkoa wa Manyara Bw. Deogratius Gallus akitoa elimu kuhusu kazi za Baraza kwa wananchi wa Kata ya Mwada, Babati mijini, mwezi Juni, 2024. Picha zote na Mpigapicha Wetu



Mjumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Mkoa wa Singida Bi. Theresia Mande (kulia) akitoa elimu kuhusu umuhimu wa kutunza miundombinu ya maji na umeme ili iwe endelevu kwa maslahi ya jamii. Bi. Mande aliwaomba wana klubu hao kuwa mabalozi wa EWURA CCC katika makazi yao.. Picha na Mpigapicha Wetu

Waombwa kuwa mabalozi wa Baraza

Na Geofrey Sokesia, Singida

Wanamichezo wa klubu ya mpira wa miguu ya Mirumba wameombwa kuwa mabalozi wa Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati maji (EWURA CCC) ili jamii iweze kutambua haki na wajibu wao kama watumiaji wa huduma za nishati na maji kupitia michezo wanayoifanya.

Wito huo umetolewa hivi kari-buni na Bi. Theresia Mande ambaye ni Mjumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji mkoa wa Singida (RCC) wakati Kamati hiyo ilipotembelea na kutoa elimu kwa vijana wanamichezo wa klubu ya mpira wa miguu ya Mirumba yenye masikani yake mtaa wa Jinery Singida.

Bi. Mande aliwaomba vijana hao kuwa mabalozi wa kusambaza elimu inayomhusu mtumiaji wa huduma za nishati na maji kupitia jukwaa la michezo akiamini kuwa wanamichezo ni mongoni mwa jamii inayotumia huduma za nishati na maji lakini pia michezo

ni jukwaa mojawapo la kutolea elimu.

"Ninyi wanamichezo vijana mnaweza mkatusaidia kusambaza elimu na taarifa kuhusu huduma za nishati na maji kwa jamii inayowazunguka kupitia nafasi mliyonayo katika michezo," alisema Theresia.

Bi. Mande aliendelea kusema "Naamini mara nyingi klubu yenu upata nafasi ya kushiriki katika mashidano mbalimbali ambapo wakati mnashiriki michezo hiyo mnaweza kutumia jukwaa hilo kugawa vipeperushi kwa mashabiki na wapezi wa mpira wa miguu wanaokusanyika kwa ajili ya kutazama michezo huu."

Bi. Mande alisema anaamini kuwa siku za mechii huwa kunakuwa na kundi kubwa la watazamaji hivyo aliwaomba vijana hao kutumia muda wao kidogo kutoa elimu hata kwa kuwagawia vipeperushi watazamaji hao.

Lakini aliwaambia wanamichezo hao kuwa wanaporudi majumbani kwao wawape wanajamii elimu hiyo ambayo wao wamepewa siku hiyo. Kwa kufanya hivyo watakuwa wameli-saidia Baraza kufikisha elimu kwa wa-

nanchi na kuwa msaada kwa jamii.

Aidha Bi. Mande aliwaomba wana michezo kuititia uongozi wao kuialika ofisi ya EWURA CCC Mkoa wa Singida pale wanapokuwa na mashindano yanayoshirikisha klubu zingine ili iweze kutumia jukwaa hilo kutoa elimu ya mtumiaji wa huduma za nishati na maji.

Kwa upande wake mmoja wa viongozi wa klubu hiyo Bw. Burhani Haji alisema kuwa klubu yake imepokea kwa moyo mmoja ombi la kuwa balozi wa hiari katika kushiriki kuhamasisha na kutoa elimu kwa wananchi wa maeneo ambayo klubu yao inafanya michezo yake.

Bw. Haji alisema wao wanayo fursa nzuri ya kukutana na vijana wenzao hasa nyakati za michezo na hivyo kuweza kuwapa elimu juu ya shughuli za Baraza na kazi zake lakini pia elimu kuhusu wajibu na haki za watumiaji wa huduma za nishati na maji.

"Tutajitahidi kuwahamsisha vijana wenzetu ili waweeze kupokea na kusambaza elimu hii kwa jamii kwa kuwa tumetambua nafasi yetu na umuhimu wa elimu hii katika jamii yetu," alisema Bw. Haji.

Mwisho, aliahidi kutoa ushirikiano wa dhati kwa Baraza kwa kutoa taarifa pale watakapoona kuna changamoto zozote zinazohusu huduma za umeme, maji, mafuta pamoja na gesi katika maeneo wanayoishi.

Wajasiriamali wanawake walishukuru Baraza kwa kuwapa elimu

Na Magreth Temba, Ruvuma

Wanachama wa vyama vya wajasiriamali wanawake wa Manispaa ya Songea wamelishuku-ru Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) kwa kuwapa elimu kuhusu huduma za nishati na maji.

Pongezi hizo zilitolewa wakati wa mukutano uliofanyika mapema Juni 2024, ambapo EWURA CCC ilitoa elimu juu ya haki na wajibu wa watumiaji wa huduma hizo. Katika mukutano huo, wajasiriamali walijifunza jinsi ya kuwasilisha malalamiko yanayohusu huduma za nishati na maji pindi wanapopata huduma zisizokidhi matarajio yao.

Akiongea kwa niaba ya wajasiriamali wenzake, Bi. Rehema Nyoni, alii-pongeza EWURA CCC kwa kutambua umuhimu wa kundi hilo na kuhakikisha wanapata elimu inayosaidia ku-

wajengea uelewa katika matumizi ya huduma za maji na nishati.

"Naishukuru EWURA CCC kwa kuhakikisha makundi haya ya wajasiriamali wanawake yanapata elimu am-bayo itatusaidia katika matumizi yetu ya huduma za nishati na maji. Naamini kutokana na wasilisho hili kila mmoja wetu hapa amepata kitu, hivyo sasa tutakuwa na uwezo wa kutambua cha kufanya ili tupate huduma bora," alise-ma Bi. Nyoni.

Alifanua kuwa kabla ya kupati-wa elimu hiyo, walikuwa wakitumia huduma za nishati na maji bila ufahamu wa kutosha, na walipokumbana na changamoto hawakujua pa kupeleka malalamiko yao. Lakini sasa, baada ya elimu hiyo, wanajua wapi pa kukimbilia pindi wanapokuwa na malalamiko.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji mkoja wa Ruvuma, Bw. Edmundi Mnyawami, aliwhahakikisha wajasiriamali hao kuwa Kamati inafanya kazi na

makundi yote bila ubaguzi, na kwamba kila mtu anastahili kupata elimu na fursa ya kutoa malalamiko pale asi-poridhishwa na huduma anazopata.

Mnyawami alieleza kuwa, ueli-mishaji huo umelenga kutoa uelewa mzuri kwa wajasiriamali kuhusu huduma zinazodhibitiwa na EWURA na kujuu namna sahihi ya matumizi ili pamoja na mambo mengine, kuepuka bili kubwa zisizo za lazima, pamoja na kulinda miundombinu dhidi ya uharibifu. Alisisitiza umuhimu wa kuwfundisha wengine elimu walio-pata ili kuwa na jamii yenye uelewa kuhusu huduma za nishati na maji.

"Nawaombeni sana akina mama, kila aliyepata elimu hii amfundishe na mwenzake au amwelekeze kufika katika ofisi zetu kujifunza zaidi ili hati-maye tuwe na jamii yenye uelewa juu ya huduma za nishati na maji," alisema ndugu Mnyawami.

Mwisho, Mnyawami aliomba kundi hilo la wanawake kuendelea kushirikiana na Baraza ili liweze kutoa elimu zaidi kwenye mikutano yao, kwani kufanya hivyo kutasaidia wanawake wengi zaidi kupata elimu hii muhimu inayohusu huduma za nishati na maji.

Shukrani



UFAHAMU MKATABA WA HUDUMA KWA MTEJA UTASITISHIWA HUDUMA YA MAJI UKIFANYA YAFUATAYO:-

- Kujiunganishia huduma ya maji kinyume na utaratibu.
- Kuharibu miundombinu ya maji au kuchepusha maji.
- Kutolipa Ankara ya maji kwa wakati.
- Kutumia maji wakati mita imesimama
- Kuwazuia/kumzuia watumishi wa TUWASA kufanya ukaguzi wa miundombinu ya maji kwenye eneo la mteja



**MAMLAKA YA
MAJISAFI NA USAFI WA
MAZINGIRA SONGEA (SOUWASA)**

**JE? UNACHANGAMOTO/TAARIFA INAYOHUSU HUDUMA
YA MAJI KWENYE MTAAWAKO**
**PIGA SIMU ZA BURE 0677091360 (MASAA 24)
NA 0800110010 (SAA 1:30 ASUBUHI – 11:00JIONI)**
AU
**WASILIANA MOJA KWA MOJA NA MAFUNDI KUPITIA NAMBA
ZIFUATAZO HAPA CHINI:**

NO	JINA	ENEO LA KAZI	NAMBA ZA SIMU
01	ALEX KAPONGO MAGRETH HAULE	MSHANGANO UPANDE WA JUU KULIA, MAKING'INDA, GASSA.	0677083374 0677083390
02	RAJAN KASSIM	MSHANGANO UPANDE WA JUU KUSHOTO, BOMBAMBILI, MKUZO, OSTERBAY, GASSA KUSHOTO.	0677083364
03	PHILIP MWINGIRA JASMINI HAMISI	MATARAWE, MJIMWEMA YA KULIA	0677085774 0716912306
04	LUNAS MCHATTA BARAKA MNGWILA	RUVUMA, MAJENGO, MJINI, MFARANYAKI	0677083369 0712348837
05	COSMAS KOMBA GEOFREY NGONYANI	MKUZO, MALIASILI, MWENGEMSHINDO MITENDEWAWA	0677083381
06	GODFREY MAPUNDA RENATUS ASSENKA	MATEKA, MAKAMBI, MPAMBALYOTO, NDILIMA LITEMBO	0659624155 0677083368
07	TEMSI MAPUNDA RENFRIDA MAPUNDA	LIZABONI, RUHUWIKO	0625297765 0677083368
08	SILVERIUS HYERA YAHAYA MAPUNDA	MATOGORO, MLETELE, PAMBAZUKO	0615230685 0677083371
09	MANAF RASHID	LIKUYUFUSI, LILAMBO	0753008186


JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAJI
MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA BABATI


WASILIANA NASI
0677-025-537

HUDUMA KWA WATEJA

**Mamlaka Inaomba
ushirikiano wako katika
Kuhakiki Usomaji wa Mita
yako Pindi Upatapo
SMS ya Usomaji wa Mita**

**ZOEZI LA
USOMAJI**

MITA ZA WATEJA

**Kila Mwezi Kuanzia
Tar 10 - 19**

**HAKIKI USOMAJI
WAKO**

**LIPA BILI YAKO KWA
WAKATI KUEPUKA
USUMBUFU WA
KUSITISHIWA HUDUMA**

Huduma Kwa Mteja
0677-025-537

Maswali yaulizwayo mara kwa mara

Maswali na Majibu

Swali: Je, TANESCO wanafidia kiasi gani kwa mtu aliyekufa sababu ya umeme?

TANESCO hawamfidii mtu ambaye ni marehemu. Kwa mujibu wa Kanuni ya 24(1) na (2) ya Kanuni za Shughuli za Uzalishaji, Upelekaji, na Usambazaji Umeme za mwaka 2023 imeelekeza kuwa, anayeweza kufidiwa ni mtu aliy-eumia au kupoteza mali zake

Swali: Je, ni mambo gani TANESCO wakifanya wanaweza kufutiwa au kusimamishwa leseni na EWURA?

Kanuni ya 17(1) (a) (b) na (c) ya Kanuni za Shughuli za Uzalishaji, Upelekaji, na Usambazaji Umeme za mwaka 2023 inatoa sababu kuu 3:-

1. Ukiukwaji wa masharti ya leseni
2. Ukiukwaji wa masharti ya sheria na kanuni
3. Mwenye lesseni kushindwa kulia-pa tozo za kiudhibiti

Swali: Je ni vituo gani sahihi vya kununua mafuta?

Nunua mafuta katika vituo vya mafuta vilivyopewa leseni na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (EWURA), Rejea Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015 kifungu namba 131(4) Sura ya 392.

Swali: Je nifanye nini kama sijaridhishwa na ukaguzi wa mita ya umeme uliofanywa na TANESCO katika nyumba yangu?

Kanuni ya 8 ya Kanuni za Jumla za Umeme za mwaka 2020 Tangazo la Serikali na. 945 imeweka wazi kuwa kama mteja hajadhirika na ukaguzi uliofanywa na TANESCO anaweza kupeleka lalamiko lake EWURA ndani ya siku 14 toka ukaguzi ulipofanyika.

EWURA itatoa amri ya kufanyika ukaguzi mpya chini ya msimamizi wa ukaguzi anayejitegemea, na kama itathibitika kwamba ukaguzi wa kwanza

ulikuwa sahihi basi mteja atagharamia na kwamba iwapo itagundulika kuwa ukaguzi haukuwa sahihi basi gharama za ukaguzi huo zitakua za TANESCO.

Swali: Mamlaka za maji zinawezaje kusaidia watu wasiojiweza kiuchumi kupata huduma ya maji safi?

Sheria ya Maji ya mwaka 2019 kifungu namba 23(1) kinazitaka mamlaka zote za maji nchini kuzingatia uwepo wa mahitaji ya wasiojiweza kiuchumi katika utoaji huduma za maji safi na usafi wa mazingira.

Kifungu cha 23(2) cha Sheria ya Maji ya mwaka 2019 kinazitaka mamlaka za maji kushirikiana na mamlaka za serikali za mitaa kuwatambua watu wasiojiweza kiuchumi na kuwasaidia kupata huduma za maji

Swali: Je, kama mtumiaji yupo daraja la watumiaji wadogo (D1) akahamishwa daraja la kawaida (T1) anatakiwa kusubiri muda gani kuomba kurudishwa daraja la watumiaji wadogo (D1) toka alpohamishwa?

Amri ya marekebisho ya bei ya TANESCO mwaka 2016 (TANESCO Tariff Adjustment Order 2016 GN. 119/2016) mteja akihamishwa toka Daraja la watumiaji wadogo (D1) kwenda watumiaji wa kawaida (T1) uhamisho huo utakuwa wa moja kwa moja (Permanent)

Swali: Je, nyumba zote zinapaswa kulipia kodi ya majengo?

Sheria ya Fedha ya mwaka 2016, Sheria ya Fedha ya mwaka 2017 na Mabadiliko ya Sheria mbalimbali (The Written laws (Miscellaneous) Amendments Act No. 2 Februari, 2019 imetaja majengo yasiyotozwa kodi ambayo ni pamoa:-

Kibanda cha udongo, nyumba za nyasi na makuti na nyumba za matope na udongo, na zinazofanana na hizo.

Maswali yaulizwayo mara kwa mara

Swali: Je, ni hatua gani za kufuata ikiwa mteja anataka kupimiwa dira yake ya maji kutokana na mashaka ya ufanisi wa dira hiyo?

Kanuni ya 51(1) (2) (3) ya Kanuni za Usambazaji Maji za 2019 GN 828, mteja atafika ofisi za mamlaka ya maji na kuomba kupimiwa mita yake na atatakiwa kulipa gharama za kupimia ambazo atajulishwa akifika katika ofisi hizo.

Mteja atapatiwa namba ya malipo, na endapo mita hiyo ikathibitika kuwa iko sahihi, mteja hatarudishiwa pesa aliyolipa na ikionekana mita ni mbovu atarejeshewa pesa aliyolipia.

Swali: Je, ni nani anayewajibika kulipia gharama za kuhamisha dira ya maji ili iwe jirani na makazi ya mteja?

Kwa mujibu wa Kanuni ya 39(1) (c) ya Kanuni za Maji, Ubora wa Huduma na Leseni za 2020, GN. 849, mita zote za maji hufungwa karibu na eneo la mteja na mteja anatakiwa kushuhudia mita ilipo baada ya kufungwa ili kujiridhisha na usalama,

Haitakiwi mita kuwa mbali na makazi ya mteja na ikithibitika mita ipo mbali na makazi ya mteja basi mamlaka ya maji itawajibika kusogeza mita karibu na mteja.

Swali: Je, mamlaka ya maji inaweza kufunga mita kwa mteja aliyechimba kisima kwa matumizi ya maji nyumbani?

Hapana! Mamlaka za maji hufunga mita kwa wateja waliounganishwa kwenye huduma za maji safi na ma-jitaka zinazotolewa na mamlaka hizo tu. Rejea Kanuni ya 52(3) ya Kanuni za Maombi ya Bei na Upangaji wa Gharama za mwaka 2020 (The Water Tariff Application and Rates Setting Rules, 2020 GN No.490.

Swali: Nani anayefuatilia kuhakikisha uzito ulioandikwa katika mtungi wa gesi ni sahihi ili kuepukana na udanganyifu kutoka kwa dealers?

Kifungu cha 19 cha Sheria ya Vipimo Sura ya 340 inataka vipimo vyote kuthibitishwa na Wakala wa Vipimo.

Swali: Bomba la maji linapoharibika ni wajibu wa nani kulitengeneza?

Kwa mujibu wa Kanuni ya 39(1) (b) ya Kanuni za Maji na Usafi wa Mazingira, Ubora wa Huduma na Leseni, za mwaka 2020, GN 849, zinabainisha kuwa, kama bomba limeharibika kabla ya mita ya maji na uharibifu huo hautokani na mteja/mtumiaji, ni wajibu wa mtoa huduma kutengeneza. Ni wajibu wa mteja kama uharibifu huo umetokea baada ya mita

Swali: Je ni kweli kuwa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira huruhusiwa kukadiria bili za wateja wao?

Ni kweli Mamlaka za majisafi na usafi wa mazingiraz inaweza kukadiria bili ya mteja.

Kanuni ya 42 (2) ya Kanuni za Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira, Ubora wa Huduma na Leseni za mwaka 2020, GN 849, inaeleza kuwa, endapo mita ya maji ya mteja itakuwa mbovu, mamlaka itaandaa bili ya mteja huyo kwa kutumia wastani wa usomaji wa matumizi yake ya maji wa kipindi cha miezi mitatu ya nyuma.

Swali: Je ni kweli kuwa mteja wa maji inapotokea bili kuwa kubwa na akashindwa kulipa kwa mkupuo anaweza kuiomba mamlaka kulipa bili yake hiyo kidokidogo?

Ni kweli! Kanuni ya 52 (1) ya Kanuni za Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira, Ubora wa Huduma na Leseni za mwaka 2020, GN. 849 inaeleza kuwa,

Maswali yaulizwayo mara kwa mara

Maswali na Majib

mtohuduma anaweza kumpangia mteja wa maji namna ya kulipa bili yake kwa awamu kutokana na uwezo wake wa kulipa. Malipo hayo yatalipwa kwa awamu kwa kipindi kisichozidi miezi sita, lakini pia Kanuni ya 52 (2) inaeleza kuwa, kipindi hicho mteja atatakiwa pia kulipa bili zake zote mpya pamoja na deni lake, kushindwa kufanya hivyo itampelekeea kukatiwa huduma ya maji.

Swali: Je, ni kwa nini vituo vya mafuta vinauza mafuta yale yale lakini bei tofauti tofauti?

Vituo vya mafuta vimepewa uhuru wa kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani lakini havitakiwi kuvuka bei kikomo (price cap) ambayo imewekwa na mdhibiti (EWURA).

Swali: Je, ni muda gani EWURA wanatan-gaza bei za mafuta?

Kanuni za Upangaji wa bei za Mafuta za mwaka 2020 (5) (2) za EWURA, bei elekezi za mafuta zinatoka kila Jumatano ya mwanzo ya mwezi husika katika magazeti mawili ya Kiswahili na mawili ya Kiingereza, ambayo yanapati-kana kiurahisi kwa wananchi.

Wananchi wanaweza kupata bei elekezi za mafuta kuitia kwenye simu zao kwa kupiga *152*00* au kuitia tovuti yao ambayo ni www.ewura.go.tz

Swali: Endapo rimoti ya mita yangu imeibiwa au mpangaji ameondoka nayo, je natakiwa kufanya nini kuendelea kupata huduma ya umeme?

Kwa mujibu wa kituo cha huduma kwa wateja TANESCO Makao Makuu, "rimoti ya mita kwa jina la kitaalamu, "Customer Interface Unit" (CIU) inapoi-biwa au kupotea, mteja anapaswa kutoa taarifa kituo cha polisi ili kupatiwa fomu ya kutolea taarifa ya upotetu "Loss

Report Form".

Baada ya hapo mteja ataandika barua kwenda kwa Meneja wa TANESCO katika mkoa husika huku akiambatani-sha taarifa ya upotetu kutoka Polisi.

TANESCO itafanya uchunguzi kwa kuitia wataalam wake na mara baa-da ya kujiridhisha mteja ataruhusiwa kulipia "CIU" mpya na gharama itatege-me aina ya kifaa hicho kwamba ni kwa mteja wa umeme wa njia moja (Single phase) au njia tatu (Three phase).

Swali: Je, taasisi au viwanda wanaweza kulalamikia huduma mbovu zinazodhibitiwa na EWURA?

Ndiyo! Kulingana na Kanuni ya 4(1) ya Kanuni za Taratibu za Kutatua Migogoro za EWURA za Mwaka 2020, mtu yeoyote nayatumia huduma zinazodhibitiwa na EWURA anaweza kuwasil-ishia malalamiko EWURA dhidi ya mto huduma anayedhibitiwa. Pia, Kanuni ya 4(2) imeipatia nguvu EWURA CCC ya kuwasilisha malalamiko kwa niaba ya mlalamikaji.

Swali: Je, mtumiaji ni nani kwa muktad-ha wa huduma zinazotolewa na EWURA CCC?

Mtumiaji ni mtu, taasisi, kiwanda au kundi la watu ambao wameshawahi kutumia au wanaotumia huduma au bidhaa zinazodhibitiwa na EWURA, kwa ajili ya matumizi binafsi na siyo kwa kufanya biashara (kuuza).

Swali: Je, kuna uwezekano mita ya TANESCO kuiba au kupunja token ili ziishe mapema/ haraka?

Hapana! Unachokinuna ndicho unachokitumia. Kuna visababishi vya umeme kuisha haraka ambavyo ni pamoja na uchakavu wa miundombinu ya umeme katika jengo la mteja, au matumizi makubwa ya mteja.



Nukuu Maridhawa

“

Moja ya shughuli za Baraza ni kuzishauri mamlaka za maji nchini ambapo moja ya eneo ambalo Baraza kwa muda mrefu sasa limekuwa likisisitiza ni umuhimu wa mamlaka za maji kuwafungia wateja wake mita za malipo ya kabla

-- *Katibu Mtendaji wa EWURA CCC,
Bi Stella Lupimo*

“

Nawapongeza kwa kazi kubwa mnayofanya katika jamii ya Tanzania. Ninaelewa na kutambua shughuli zenu na nimeduwa nikiona machapisho yenu mara kwa mara Bungeni. Ni muhimu kuendelea kufanya kazi kwa bidii na uadilifu ili kufikia malengo ya kuanzishwa kwa Baraza.

-- *Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati
Mhe. Dkt. Doto Biteko*